# NAFASI YA WANAWAKE KATIKA UHIFADHI WA MAZINGIRA KATIKA RIWAYA YA *NAKURUTO*: MTAZAMO WA FASIHI YA UFEMINISTI WA KIEKOLOJIA.

NA

SABULA A. MILLICENT

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI WA SANAA KATIKA KISWAHILI.

University of NAIROBI Library
0377563 2

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

© 2014

# UNGAMO

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya shughuli yoyote ile wala kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu chochote kile."

______________________ 17. 11. 2014

SABULA A. MILLICENT

(Mtahiniwa) (Tarehe)

"Tasnifu hii imeandikwa, kutolewa na kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa chuo kikuu."

______________________ 18/Nov/2014

DKT. ZAJA OMBOGA

(Msimamizi) (Tarehe)

______________________ ______________________

DKT. MWANGANGI WA MUSYOKA

(Msimamizi) (Tarehe)

## TABARUKU

Mume wangu mpendwa Josiah Agweny,

Mfadhili wangu masomoni,

Ishara ya wema ni ipi?

Aaah! Shukrani yashinda mengine yote.

## SHUKRANI

Shukrani zangu za mwanzo ni kwa Mola Maulana; uhai amenitunuku afya njema kanipa niweze kutenda yote haya. Wema na fadhili zake zimekuwa pamoja nami. Aidha, nawashukuru wahadhiri wangu ninaowadhamini katika Idara ya Kiswahili hasa wale walionifunza darasani na kuhakikisha masomo yangu ya uzamili yamekamilika kwa wakati uliofaa. Wahadhiri hao ni: Prof. Abdulaziz, Prof.Mbatiah. Prof.Wamitila, Prof. Habwe, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof.Kithaka wa Mberia, Dkt. Mukhwana, Dkt. Swaleh, Bw. Mungania, Dkt. Olali na Dkt. Buregeya. Nawashukuru Dkt. Zaja na Dkt. Mwangangi wa Musyoka ambao walihakikisha kazi yangu imekamilika.

Kamwe, siwezi kumsahau rafiki Nabeta Sangili kwa msaada alionipa masomoni hasa vitabu na makala niliyotumia almuradi nifaulu. Mchango wake katika kufaulisha shahada yangu hauhesabiki. Sitasahau mjomba Bw.Jethron Ayumba ambaye ni mhadhiri chuo cha Maseno kwa motisha aliyonipa ili niendeleze masomo yangu kwa faida yangu ya baadaye. Shukrani zangu kwake Vivian Hongo mfanyikazi katika maktaba ya chuo kwa usaidizi wake na uongozi katika utafiti wangu. Vilevile kwa darasa zima la M.A mwaka 2012 kwa ushirikiano wao hata kazi zilipotuzonga.

Mwisho ni kwa familia yangu: Mume wangu aliyejitolea kunifadhili, kunihimiza na kunipa mawaidha. Pia, watoto wangu Jessil na Jakes walionivumilia wakati wangu wote wa masomo. Heshima ni kwa mama mzazi Jesicah ambaye kila wakati aliniombea ili nifaulu kutamatisha shahada ya uzamili. Nani kama nyinyi! Mola awakirimu. Ahsanteni sana.

Kwa wale wote niliowataja na wale sikuweza kuwataja, nawaombea kila la heri maishani mwenu.

# IKISIRI

Fasihi ya kiekolojia ni uwanja uliochipuka miaka ya 1970 na kuendelea miaka ya 1990 kuchanganua, kuchambua na kuhakiki kazi za kifasihi. Uwanja huu unalenga kuangazia fani na maudhui katika matawi ya fasihi kiekolojia kama vile ya Kiafrika, Kimarekani na Kifeministi. Utafiti huu unahusu nafasi ya wanawake katika uhifadhi wa mazingira kwa mtazamo wa fasihi ya ufeministi wa kiekolojia. Lengo kuu la utafiti huu ni kupambanua mchango wa ufeministi wa kiekolojia katika fasihi ya Kiswahili. Utafiti huu uliongozwa na madhumuni haya: kubainisha mchango wa ufeministi wa kiekolojia katika uhifadhi wa mazingira katika riwaya ya *Nakuruto*; kupambanua mhusika Nakuruto na mchango anaoutoa katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira; kujadili kwa kina changamoto anazopitia mwanawake katika kuhifadhi mazingira; kujadili athari za masuala ya kimazingira na jinsi zinavyojitokeza katika riwaya. Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni nadharia ya Ufeministi wa kiekolojia iliyoasisiwa na mfaransa Francoise d'Eaubonne mwaka wa 1974. Nadharia hii ilibuniwa kwa ajili ya kuleta mapinduzi ya kiekolojia hasa kwa kumzingatia mwanamke. Utafiti huu ulifuata muundo wa uchanganuzi wa makala ambapo maelezo yetu yaliangazia masuala tata yaliyoko kwenye matini tuele. Makala ya kimsingi ya utafiti yalikuwa ni riwaya ya *Nakuruto* ilhali makala ya sekondari yalitokana na usomaji wa vitabu na makala yaliyohusu mada. Utafiti huu ulibainisha kwamba ufeministi wa kiekolojia una nafasi ya kuwazindua wanawake ili kuleta ukombozi wa kimazingira. Aidha, utafiti ulitambua kuwa mhusika Nakuruto aliwazindua wanajamii kupitia kwa elimu na maarifa yake ya kimazingira, hivyo kusababisha mapinduzi. Utafiti ulitambua kwamba wanawake wanasimangwa, kutukanwa, kudharauliwa na kudunishwa wanapojihusisha na harakati za utunzaji mazingira. Mwisho utafiti ulitambua kwamba umaskini, kukauka kwa chemichemi za maji, uskwota, magonjwa na vifo ni athari zinazosababishwa na uharibu wa mazingira. Utafiti huu ulihitimisha kwamba mwanamke anastahili kupewa nafasi katika uhifadhi wa mazingira na kwamba, fasihi ya Kiswahili ina uwezo wa kumulika masuala ya kielokojia kama yanavyojitokeza katika jamii. Kwa kuwa utafiti huu haukuweza kuchunguza vipengele vyote vya kifasihi mazingira, mtafiti anapendekeza kwamba utafiti wa baadaye uzingatie mikabala mingine kama vile fasihi mazingira kieneo, Kiafrika na Kimagharibi, hasa kwa mkondo wa kilinganishi.

YALIYOMO

Ungamo....................i

Tabaruku....................ii

Shukrani....................iii

Ikisiri.................... iv

Yaliyomo....................v

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

1.1 Usuli wa utafiti....................1

1.2 Tatizo la utafiti....................4

1.3 Sababu za uteuzi wa mada....................5

1.4 Madhumuni ya utafiti....................5

1.5 Nadharia tete....................6

1.6 Upeo na mipaka ya utafiti....................6

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada....................7

1.7.1 Fasihi ya kiekolojia....................7

1.7.2 Ufeministi wa kiekolojia....................12

1.7.3 Wanawake na mazingira....................14

1.8 Misingi ya kinadharia....................17

1.8.1 Upungufu wa nadharia....................23

1.9 Mbinu za utafiti....................24

SURA YA PILI: SWALA LA KIMAZINGIRA KATIKA FASIHI ANDISHI

2.1 Utangulizi....................25

2.2 Tungo za kimazingira....................25

2.3 Muhtasari wa riwaya ya *Nakuruto*....................28

2.4 Hitimisho....................30

SURA YA TATU: MCHANGO WA UFEMINISTI WA KIEKOLOJIA

3.1 Utangulizi....................31

3.2 Ufeministi wa kiekolojia....................31

3.2.1 Uzinduzi....................32

3.2.2 Ukombozi....................35

3.2.3 Matatizo ya wanawake....................37

3.3 Pingamizi katika uhifadhi....................41

3.4 Hitimisho....................43

SURA YA NNE: UHARIBIFU WA MAZINGIRA NA ATHARI ZAKE

4.1 Utangulizi....................44

4.2 Uharibifu wa mazingira....................48

4.2.1 Ubinafsi....................48

4.2.2 Teknolojia na viwanda........50

4.2.3 Ukoloni........53

4.3 Athari za uharibifu wa mazingira........58

4.3.1 Athari kwa mwanadamu........59

4.3.2 Athari kwa wanyama na viumbe wengine........66

4.3.3 Athari kwa maliasili na bioanuwai........68

4.4 Hitimisho........70

SURA YA TANO: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1Hitimisho........71

5.2 Muhtasari........71

5.3 Kuhusu nadharia tete........72

5.4 Mapendekezo kuhusu utafiti zaidi........73

MAREJELEO........75

VIAMBATISHO........80

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Usuli wa utafiti

Uhakiki wa ufeministi wa kiekolojia unahusu kuchunguza kazi za kifasihi kwa kuzingatia mtazamo kike unaolenga zaidi kwenye maswala ya ekolojia. Utafiti huu ulijishughulisha na kuchunguza jitihada anazofanya mwanamke kuhakikisha kuwa amekomboa mazingira yake kutokana na uharibifu. Katika kukomboa mazingira haya mwanamke anakumbana na pingamizi mbalimbali zenye nia ya kumfisha roho na kuona uwanja huu kama wa mwanamume. Katika harakati za kurejesha uhai wa mazingira lazima mwanamke aweze kutafuta mbinu zitakazowasaidia wanawake wengine wanaotatizika wakati mazingira yanapozorota hasa tunapoangazia riwaya ya *Nakuruto* ya Clara Momanyi. Kabla ya kushughulikia riwaya, lazima tuelewe hali ya ekolojia yetu na matendo mbalimbali yanayozua matatizo kwenye mazingira na ikiwa pamekuwa na tafiti za fasihi ya Kiswahili kushughulikia

Ekolojia yetu imo katika hali ya hatari ya maangamizi kutokana na matendo ya kibinafsi ya kibinadamu. Matendo kama vile: kukata miti, kujenga nyumba katika maeneo oevu, kuongezeka kwa teknolojia haribifu za kisasa na ukosefu wa uongozi adilifu katika masuala ya ekolojia, yamesababisha mitandao ya viungauhai kudhoofika. Mwisho wa matendo haya ni kwamba jotohewa limeongezeka na kuvuguta sayari yetu, magonjwa yamezidi, vifo vimekithiri na mazao katika jamii zetu yamepungua hivyo kusababisha njaa. Athari hizi zinatatiza maisha ya binadamu na maendeleo endelevu.

Miaka ya hivi karibuni, wataalam wa angahewa, ekolojia na pia waandishi wamejitokeza kuzindua wanadamu wote katika sayari ya leo kuhusu tata za kiekolojia zinazomkabili

mwanadamu. Kando na makundi haya makongamano mbalimbali yameundwa kuweza kutatua shida hizi za kiekolojia. Mojawapo wa kongamano kuhusu mazingira ni lile la shirika la umoja wa kimataifa kuhusu mazingira na maendeleo (UNCED) lililofanyika Rio de Janeiro Juni 14 mwaka wa 1992 ambalo linajulikana kama Agenda 21. Kongamano hili lilikuwa na madhumuni ya kusitisha na ikiwezekana kupunguza athari zinazotokana na kudorora kwa mazingira ili kuendeleza maendeleo yasio na athari kwenye mazingira katika mataifa yote. Kilichochochea mpango huu ni kwamba sheria zilizoko zinagawanya mataifa na kuongeza kiwango cha umaskini, njaa na magonjwa dunia nzima na ambazo husababisha kuendelea kuzorota kwa mifumo ya ekolojia ambayo ndiyo uhai wetu.

Kupitia ung'amuzi muhimu kwamba utegemezi mkubwa upo kwenye dunia tunamoishi, kongamano hili lilitoa misingi muhimu ya kimazingira baadhi yake ikiwa: ili kufikia maendeleo endelevu,uhifadhi wa mazingira utabaki kuwa sehemu muhimu katika mchakato wa maendeleo, mataifa yawe na sheria faafu za kimazingira, mataifa yaweze kuunda sheria ya kitaifa kuhusu fidia kwa wahasiriwa wa uchafuzi wa hewa na matatizo mengine ya kimazingira, wanawake wana jukumu muhimu katika maendeleo na utunzaji wa mazingira hivyo kujumuishwa kwao ni jambo la busara katika kufikia maendeleo endelevu. Hii ni baadhi tu ya misingi muhimu iliyojadiliwa ingawa utunzaji mazingira ndilo lililokuwa wazo kuu ili kuepuka madhara ambayo yaliathiri kukua kwa uchumi na afya bora ya mwanadamu.Vilevile, mashirika ya kimataifa yameendelea kulipa swala hili la mazingira umuhimu mkubwa hivi kwamba yanazidi kufadhili shughuli zilizo na umuhimu katika uhifadhi mazingira.

Juhudi za uhifadhi mazingira ni lazima zitekelezwe na watu wa nyanja tofautitofauti wakiwemo wasomi na watunzi wa fasihi kando na wanasayansi ili waweze kumfikia binadamu wa tabaka la chini zaidi anayehusika nayo moja kwa moja. Fasihi huwa na lengo la kufikia jamii ili iweze

kuikosoa, kuielimisha na hata kuitahadharisha kuhusu matendo mabaya ya mwanadamu. Malengo haya huishia katika kutatua matatizo yanayojitokeza katika jamii na ambayo yanatishia uhai wa wanajamii na viumbe vilivyomo. Fasihi ina mchango wa kuhamasisha binadamu kuhusu masuala ya kimazingira hasa uharibifu unaotendwa na binadamu ndiposa watunzi mbalimbali wamejitosa uwanjani kuliandikia suala hili. Watunzi hawa ni kama vile Mbogo Emmanuel katika riwaya ya *Bustani ya Edeni* na Kithaka Wa Mberia katika mkusanyiko wa mashairi *Bara Jingine* ambapo baadhi ya mashairi yanazungumzia jinsi binadamu anavyoharibu utando wa ozoni hasa shairi la 'Ngao' Hata hivyo kila mtunzi ana mtazamo wake wa kiekolojia na jinsi ya kuukabili.

Uwanja wa fasihi mazingira ni uwanja mpana na unatanuka kadiri watunzi wanavyouandikia au kuuzungumzia katika maeneo wanamoishi,spishi mbalimbali zinazofaidika na ekolojia na hata masuala yanayohusiana na maliasili na jinsi ya kuzuia uchafuzi wa hewa. Fasihi ya Kiswahili hata hivyo haijatamba katika kulipanua wazo hili la kimazingira hivyo kusababisha kuwepo kwa tafiti chache. Utafiti uliopo ulifanywa na Arege katika mkusanyiko wa kazi za Slovic (2009). Katika kazi hizi Arege amechanganua kwamukhtasari riwaya ya *Bustani ya Edeni (2002)*, shairi la 'Namgondo' kwenye *Kichomi* (1974) na 'Johari Bamburi' kwenye *Redio na Mwezi (2005)*. Kinachobainika waziwazi katika uchanganuzi wake ni kwamba uharibifu wa mazingira una hatari zake na lazima juhudi zifanywe kuhifadhi mazingira haya.

Vierke, (2007) aliliangazia swala la mwanamke kuhusishwa na mazingira katika makala yake 'Of plants and women. A working edition of two Swahili plant poems' iliyochapishwa katika jarida la *Swahili Forum.* Alitafiti jinsi mwanamke mwenye asili ya Waswahili anavyolinganishwa na baadhi ya mimea kama vile pilipili (kwa ukali wake), maua (urembo wake unaofifia haraka) na hata minazi kwenye utendi wa "Utumbuizo wa MjeMje" na shairi la "Mtambuu". Katika utafiti huu Vierke alionyesha jinsi mazingira asilia yalivyo na umuhimu

kwenye jamii ya Waswahili na hasa walipotungia ushairi wa kale. Utafiti huu si wa kina kwani haujajikita kwenye nadharia yoyote ya kimazingira. Aidha, haujazingatia juhudi za mwanamke katika uhifadhi wake wa mazingira.

Utafiti wa Vierke na Arege unaangazia jinsi mazingira yalivyo sehemu muhimu katika utunzi wa fasihi ingawa hazishughulikii maswala yote yanayochipuka katika eneo la kimazingira au kujikita katika nadharia za kimazingira na pia juhudi au nafasi ya mwanamke katika uhifadhi wake. Utafiti wetu hivyo basi umelipa swala la kimazingira uhai mpya wa kinadharia ambao ni mwelekeo katika kushughulikia bayana uharibifu wa mazingira. Utafiti huu hivyo basi umehusisha utafiti wa kimwingiliano baina ya taaluma ya kimazingira na fasihi ya Kiswahili, hasa fasihi iliyotungwa na kuchapishwa karne ya ishirini na moja.

## 1.2 Tatizo la utafiti

Tatizo tulilolichunguza katika utafiti huu ni uchanganuzi wa mahusiko ya mwanamke katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira. Utafiti huu ulichochewa na uelewa wetu kwamba uhifadhi mazingira si jambo linalofasiriwa na kutekelezwa kwa njia zinazowiana kati ya wanawake na wanaume. Utafiti huu basi uliangazia juhudi za wanawake, changamoto wanazopitia pamoja na wito wao katika uhifadhi wa mazingira. Katika uhakiki wetu tulichunguza mchango wa ekolojia kifeministi katika uhifadhi wa mazingira.Tulichunguza vile mhusika Nakuruto anavyowakilisha wanawake katika kuhifadhi mazingira na changamoto anazopitia katika mchakato huu. Mwisho kabisa tuliaangalia athari za uharibifu wa mazingira na jiinsi zinavyojitokeza katika riwaya.

## 1.3 Sababu za uteuzi wa mada

Mada ya utafiti iliteuliwa kwa sababu uwanja huu wa ufeministi wa kiekolojia ni mpya katika fasihi ya Kiswahili hivyo basi pana haja ya kuwepo kwa tafiti mbalimbali katika fasihi ili kuupanua ipasavyo. Hivyo utafiti huu unalenga kutoa mwanga na mwelekeo katika tahakiki za fasihi ya kiekolojia katika Kiswahili. Pia utafiti huu ulilenga kuhamasisha wasomi wa fasihi wajikite zaidi katika kulenga masuala ya mazingira ambayo ndicho kitovu cha uhai wa mwanadamu. Muhimu zaidi ni kuwa, suala la uharibifu wa mazingira linahusu kila mwanadamu wa kike au kiume hivyo basi jinsi ambavyo binadamu wa kike alivyo na umuhimu katika utunzaji wa familia yake ndivyo hivyo alivyo na utunzaji wa mazingira yake ili kizazi cha kesho kifaidike. Kwa misingi hii, ni vyema wanafasihi wajumuishe wanawake katika juhudi za kumulika maswala ya kimazingira. Aidha riwaya ya *Nakuruto* imeteuliwa kwa sababu imetungwa na mwanamke. Utafiti huu ulilenga kuonyesha jinsi mwanamke anavyojisawiri au kusawiri wanawake wenzake katika mchakato mzima wa kijamii wa utunzaji mazingira yake.

## 1.4 Madhumuni ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na lengo kuu la kuchunguza kazi ya fasihi andishi yenye mtazamo wa ufeministi wa kiekolojia kwa madhumuni yafuatayo:

a) Kubainisha mchango wa ufeministi wa kiekolojia katika uhifadhi wa mazingira.
b) Kupambanua mhusika Nakuruto na mchango anaoutoa katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira.
c) Kujadili kwa kina changamoto anazopitia mwanawake katika kuhifadhi mazingira.
d) Kujadili athari za masuala ya kimazingira na jinsi zinavyojitokeza katika riwaya.

## 1.5 Nadharia tete

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

a) Ufeministi wa kiekolojia una jukumu la kuzindua jamii hasa wanawake ili kukomboa mazingira kutokana na uharibifu unaosababishwa na mifumo mbalimbali ya kijamii.

b) Mhusika mkuu Nakuruto ni kiwakilishi cha mwanamke aliyejitolea kuleta mabadiliko ya kimazingira katika jamii.

c) Ukame na njaa, vifo, umaskini, maeneo tambarare ni baadhi ya athari za kutohifadhi mazingira.

d) Wanawake wanao uwezo wa kuleta mabadiliko kimazingira, hata ingawa wanakumbana na pingamizi za kijamii, bado wana nafasi bora katika mchakato huu.

## 1.6 Upeo na mipaka ya utafiti

Ingawa masuala mengi yamejadiliwa kwenye mtazamo wa kifeministi, utafiti huu unajikita katika kuangazia fasihi ya kiekolojia hasa ya kifeministi kwani fasihi ya kiekolojia kwa ujumla ni wazo pana ambalo linahusisha matapo mengi ya wahakiki kimazingira. Ufeministi wa kiekolojia ulilenga kumpambanua mhusika Nakuruto katika riwaya ya Clara Momanyi ya *Nakuruto* kama mwanamke aliye na jukumu na nafasi pana ya kuleta maendeleo kupitia uhifadhi wa mazingira. Riwaya hii ya *Nakuruto* ni ya hivi karibuni mwaka wa (2009) wakati ambapo masuala ya uhifadhi mazingira yameteka ung'amuzi wa kitaifa na kimataifa.

## 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada

### 1.7.1 Fasihi ya kiekolojia

Fasihi ya kiekolojia ni uwanja mpya wa kuhakiki fasihi na sanaa. Mkabala huu wa uchanganuzi fasihi na sanaa huzingatia dhana za kiekolojia katika fasihi na sanaa mbalimbali ima sanaa andishi, sanaa ya kuchora au sanaa simulizi. Fasihi ya kiekolojia ni uwanja ulioendelezwa na Glotfelty, Fromm na Buell miaka ya tisini walipozindua tena uwanja wa fasihi kiekolojia katika fasihi za kilimwengu kule Marekani. Glotfelty na Fromm (1996) wanafafanua fasihi ya kiekolojia kama uhusiano baina ya kazi ya kifasihi na ekolojia; uwanja unaochukua mtazamo wa kiardhi kwa masuala ya kifasihi. Uwanja wa fasihi ya kiekolojia ni mpana na wa kina.Uwanja huu upo mintarafu ya wanadamu kujadili na kuandika na kuchanganua diskosi mbalimbali kuhusu mandhari, sehemu za dunia, spishi za viumbe hai, maliasili, na uzuifu wa uchafu wa viwandani.

Mkabala huu unanuia kutoa taswira halisi ya jinsi wasanii mbalimbali wanavyoumba upya picha za kiekolojia katika kazi zao za kisanii. Uwanja huu unadai kwamba siyo kila mtunzi wa kifasihi anahusisha ekolojia asilia katika matini yake bali ni watunzi maalum tu ambao wamebobea na kuelewa masuala ya kiekolojia katika jamii zao na wameishia kuegemea kwenye usanii wa kiekolojia. Hii ina maana kwamba, ikiwa msanii ametunga, amesimulia ama kuchora ekolojia bunilizi, hafai kuwekwa katika kundi hili kwani yeye hazingatii sayari kama ilivyo na jinsi inavyobadilika.Msanii kama huyo anajikita katika ulimwengu ambao haupo.Garrard (2007:359) anaeleza kwamba matatizo ya kimazingira yameonekana kimsingi kuwa matatizo ya kisayansi na mijadala mingi kuhusu ongezeko la joto huhusisha zaidi wana angahewa kuliko watunzi wa mashairi au hata wahakiki wa kifasihi. Kutokana na mwelekeo wake masuala haya ya

kimazingira yaweze kuwasilishwa kwa jamii kupitia fasihi kwani ndiyo huingiliana pakubwa na utamaduni wa jamii na hivyo itaweza kufikia watu moja kwa moja.

Uandishi unaoelekea kwenye mtazamo wa kiekolojia unahitaji maarifa mengi ya mwandishi kuhusu mazingira yake ndiposa Hitt (2004:124-127) katika makala "Ecocriticism and the Long Eighteeth Century" iliyochapishwa kwenye jarida la *College Literature* anaeleza kwamba ili mwandishi wa fasihi aweze kuandika kiekolojia, lazima awe na maamuzi faafu kuhusu fasihi na uharibifu wa mazingira pamoja uzorotaji unaoendelezwa na tamaduni mbali mbali za mwanadamu. Anafafanua kwamba fasihi ya kiekolojia ni mkabala unaohusiana na mitazamo mbalimbali ya kiuhakiki ambayo hujumuisha: Ufeministi, umaksi na ubaada-ukoloni na kwamba mkabala huu lazima uhusishwe na matendo yaliyopita ya mwanadamu kutokana na ongezeko la visa vya uharibifi wa mazingira. Fasihi ya kiekolojia ni mkabala ulioweza kuwasilishwa kwa wasomi ili kubaini matendo mabovu ya kibinadamu. Dhana hii iliingizwa kwenye utanzu wa ushairi katika karne ya kumi na nane ingawa wasomi wengi hawakujihusisha nayo jinsi asemavyo Hitt.Maoni ya wanamazingira yameelezwa ndani ya fasihi hasa anaponukuu kazi ya Gilpin (1891: 204-205) kuwa:

> Wakati ambapo miti inabadilishwa kuleta faida, hukatwa hata kabla ya kufikia uzuri wake. Uzuri wa karibu spishi zote za miti huongezeka inapokua na ikiwa haitabahatika kusimama mahali pasipofikika au mahali palipolindwa, hatuioni katika hali ambayo ingekuwa baada ya muda mrefu. (Tafsiri yetu)

Jukumu la fasihi ya kiekolojia ni kuleta tofauti za kimazingira kupitia maandishi yanayoangazia zaidi utunzaji na uharibifu wa mazingira. Rigby (2007) anadai kwamba fasihi ya kiekolojia inajitolea kubadili hali halisi ya uharibifu wa ekolojia kwa kuchanganua uamilifu wa kimaudhui,

kisanii, kijamii, kihistoria, kiitikadi, na kimbinu katika ekolojia asilia au vipengele vyake kama vilivyohusishwa katika fasihi au makala ya kiekolojia. Uwanja huu huangazia tanzu za kifasihi andishi na simulizi na pia katika filamu, sinema pamoja na teknolojia-burudishi. Kuna mitazamo mbalimbali ya fasihi ekolojia.Mitazamo hii ni Kama vile fasihi ekolojia Kifeministi, fasihi ekolojia Kieneo, na fasihi ya kiekolojia Kiafrika.

Maoni ya Rigby ndiyo yanayopokelewa na Nwagbara (2010:17-20) hasa akiangazia nchi ya Nigeria, Nwagbara anadai kwamba kutokana na uharibifu wa mazingira na uchafuzi wa hewa katika makazi ya watu, waandishi nchini Nigeria wanatumia sanaa kuhamasisha jamii kuhusu uharibifu huo na athari zake kwa binadamu. Nwagbara anaangazia mkusanyiko wa mashairi ya Ojaide ya *Delta Blues and Home songs* na *Daydreams ofAnts and other poems* ambayo madhumuni yake ni kuelezea uharibifu uliofanyiwa mazingira katika eneo la Delta. Nigeria ni nchi iliyo na utajiri wa mafuta na ambayo mabwenyenye wa kibinafsi hutaka kujitajirisha bila kujali athari ya uchimbaji huo kwa mazingira. Kama anvyosema Nwagbara, Ojaide anatumia njia hii ya ushairi kwa manufaa ya wanamazingira. Katika majilio ya fasihi ya kiekolojia, mashairi haya yamejali mazingira kwa kuwasilisha mahusiano ya dunia halisia na jinsi matendo ya kibinadamu yanavyoathiri ekolojia. Akinukuu shairi la "The AT & P Sapele" tunaona jinsi shairi hili ni mojawapo ya mashairi ya Ojaide linaloangazia uharibifu uliofanyiwa mimea (flora) eneo la Sapele, Niger Delta ambapo mbao zilitengenezwa kwa minajili ya kusafirishwa nchi za nje.

Mara ya kwanza kuingia AT&P

Kwa matembezi kutoka St Georges

Ilikuwa karibu na mashine ya kusaga mbao

Ardhini,

Spishi mbalimbali za miti zilinukia

Mingine kwa minajili ya kusafirishwa

Ililetwa kupitia majini

Miongo michache niliporudi nyumbani

Eneo la Delta palipojaa miti

Uwazi uliotokana na ukataji miti ulinikaribisha.

(Tafsiri yetu ; kiambatisho B)

Mazingira yameathiriwa na uchimbaji mafuta unaotajirisha wachache na kuleta athari kwenye ekolojia. Nwagbara anamwangazia Ojaide kama wakili anayemulika ukosefu wa usawa na ambao umeathiri eneo la Niger Delta. Shairi la Ojaide la "Delta Blues" katika mkusanyiko wa mashairi *Delta Blues&Home Songs* ni kiwakilishi cha maovu ya uchimbaji mafuta.

Paradiso eneo la Delta nilikozaliwa

Linalo mateso ya kiwango cha juu

Mapipa ya kemikali yatiririka

Hadi dunia nzima

Humulika maisha kwa upotovu

Urithi nilioukalia miongo mingi

Umevunjavunja nafsi na roho yangu

Uzawa wangu wanijaza maumivu makali
Yalofichwa ndani ya mapipa ya mafuta
Nakaangika utumboni mwa utajiri
Kuishi ni kwenye kitanda cha mauti
Kilichotandikwa na madalali walafi
Wavunjao amani iliyokuwepo karne hata karne
Na kuchafua sio tu mito elfu
Na hata damu yangu
Pia kuuchoma mchanga
Kutokana na wachimbaji walafi

Ndege wangu wamehamia baharini
Wanyama nao waunguzwa msituni

(Tafsiri yetu; Kiambatisho A)

Nchi za Afrika zimeathirika pakubwa kutokana na uharibifu wa ekolojia yetu hasa kukipitia: ukataji miti kiholela, uelekezaji wa taka za viwanda majini, uchafuzi wa hewa na matendo

mengine ndiposa waandishi wa fasihi hawana budi kumulika swala hili. Ojomo (2011:102), anahusisha swala la mazingira na uelewa wa Afrika hivi kwamba mazingira ya Kiafrika yamezorota na lazima mbinu mwafaka zifanywe kuyaokoa. Anaeleza kuwa matatizo haya ni matokeo ya matendo ya kibinadamu. Kama njia ya kuweza kutatua swala hili, fasihi lazima iweze kumulika maovu haya yanayofanyiwa mazingira hivyo basi pana umuhimu wa watunzi na wasomi kuchukua usukani ili kutatua matatizo hayo. Tahakiki hizi zinazua pengo katika uchanganuzi wa fasihi ya Kiswahili kwani zimejumuisha mashairi lakini utafiti wetu unaziba pengo hili kwa kulenga riwaya. Aidha makala tunayorejelea ni ya Kenya bali sio Nigeria.

### 1.7.2. Ufeministi wa kiekolojia

Ekolojia hutazama jinsi mifumo mbalimbali ya kimazingira inavyofanya kazi ili kukidhi maisha na jinsi mifumo hii inavyoharibiwa na kusababisha vifo vya mimea, wanyama na wanadamu. Ruether (1997:72-83) katika 'Ecofeminism: First and Third World Women' anaelezea ekolojia kama mfumo unaotazama jinsi mwanadamu kando na kufaidika kutokana na mazingira na maumbile asili anasababisha uchafuzi wa mchanga,hewa na maji pamoja na kuharibu uhai asilia wa mimea na wanyama na kutishia msingi wa uhai unaotegemewa na jamii za kibinadamu. Ufeministi kulingana na Wamitila (2003:253-256) ni tapo la kifalsafa ambalo linahusisha uhakiki ambao unadadisi misimamo na itikadi ya kiume na ambalo huzishambulia thamani za kiume katika fasihi. Hushambulia mitazamo ya kiume kuhusu wanawake wanavyopaswa kuhisi, kufikiri na kuitikia hali mbalimbali za kimaisha na kuona kwamba asasi ya ndoa na utamaduni ndizo zinazomkandamiza mwanamke na kumwona mwanamme kama kielelezo bora katika jamii. Hivyo basi ufeministi wa kiekolojia ni muungano wa ekolojia na ufeministi na hutaka kuongoza uhusiano kati ya wanawake na mazingira kwa kuhakiki unyanyasaji wanaopitia na

kuhimiza shughuli za uhifadhi. Hata ingawa tahakiki hizi zinagusia suala la mwanamke, wahakiki hawa hawajaonyesha nafasi ya mwanamke inavyojitokeza hasa swala la kimazingira linapowasilishwa katika fasihi ya Kiswahili ndiposa utafiti huu unapania kujaza pengo hili kwa kuangazia hasa juhudi ambazo mwanamke katika riwaya ya *Nakuruto* anafanya katika utunzaji wa mazingira.

Ruether anaendeleza wazo hili la ufeministi wa kiekolojia kama mtazamo uliojengeka kwa msingi kwamba kuna mahusiano kati ya utamaduni wa kimagharibi na utamaduni wa kibabedume,kati ya kutawaliwa kwa wanawake na kutawaliwa kwa maumbile. Haya yanamaanisha kwamba kutawaliwa kwa wanawake na kwa maumbile asilia hufanyika kwanza kwenye kiwango cha utamaduni. Utamaduni wa kibabedume unamchukulia mwanamke kama aliye karibu na maumbile au mazingira. Ukaribu huu unapigiwa upato na Moore (2008:461-465) anayeangazia kazi ya Melisa Leech (2007) ya 'Earth Mothers and Other Ecofeminist Fables: How a Strategic Notion Rose and Fell' ambaye alihusika na jukumu la ufeministi wa kiekolojia kwa kutambua nguzo kuu na wazo kwamba wanawake wana uhusiano wa kipekee na mazingira.

Ufeministi wa kiekolojia hushikilia kuwa kutawaliwa kwa miili ya wanawake na kazi za wanawake kunashabihiana na kutawaliwa kwa mazingira na maumbile hivi kwamba kuna utumiaji mbaya wa mashamba, maji na hata wanyama.Hali hii inamfanya Ruether (1997:72-83) kuzua maswali yafuatayo; Ni vipi ambavyo jinsia hii ya kike imedunishwa na ubabedume hasa kwenye mifumo ya kiuchumi, kisosholojia na kisiasa? Ni vipi ambavyo kukolonishwa huku kwa miili ya wanawake na kazi zao kunalinganishwa na upataji maliasili, Ni vipi ambavyo nafasi ya wanawake ya utunzaji watoto, wakulima, wasusi, wapishi, dobi, mameneja wa taka katika jamii na familia huwadunisha na kuwalinganisha na ulimwengu uliodunishwa?

### 1.7.3. Wanawake na mazingira

Uhusiano uliopo baina ya wanawake na mazingira uliimarishwa kimataifa katika kongamano la nne la umoja wa kimataifa lililohusu wanawake kule Beijing mwaka wa 1995 ambalo lilitaka maswala ya kimazingira yatiliwe nguvu kupitia kwa harakati za maendeleo za wanawake jinsi asemavyo Buckingham (2003:6-8). Warren (2000:2-14) anachukulia swala hili la wanawake na mazingira na ekolojia kama lililotokana na uangamizaji wa misitu katika maeneo mbalimbali duniani.Wanawake walichukua jukumu la kulinda miti, misitu na kuimarisha upandaji miti. Warren anaeleza kwamba mwaka wa 1974 wanawake ishirini na saba wa Reni kaskazini mwa India eneo la Indian Garwhal Himalayas walichukua jukumu la kusitisha ukataji miti. Walitishia kukumbatia miti yote iwapo ingekatwa kwa madhumuni ya kibiashara. Maandamano yaliibuka ambayo ni vuguvugu la "Chipko" au "ukumbatiaji miti" vuguvugu ambalo lilihamasisha jamii kwamba ukataji miti kwa minajili ya biashara ulisababisha uharibifu wa miti asili hivi kwamba ilikuwa ikiondolewa na badala yake spishi za kisasa kuchukua mahala pake. Ni wazi katika kazi ya Moore (2008) kwamba wanawake hawa wa vijijini walitaka kuwasilisha athari mbaya za kimaendeleo hasa kwenye wanawake wa vijijini.

Utegemezi wa wanawake kwenye mazingira na ekolojia unadhihirika kupitia kujihusisha kwao na kilimo. Warren anatolea mfano wa wanawake wa Afrika ambao wanazalisha asilimia sabini ya chakula Afrika bila teknolojia za kisasa. Akirejelea shairi la Okot P' Bitek la 'Song of Ocol', ni wazi kwamba lazima lalama za wanawake zitiliwe maanani hasa matendo hatari ya kibinadamu kwenye mazingira ambayo yanawaathiri. Katika shairi, P' Bitek anaeleza:

Mwanamke wa Africa

Mfagiaji

Mkandika sakafu na kuta

Udongo mweusi na choo cha ng'ombe kutumika

Mpishi, mtoto mgongoni mwosha vyombo

Mpandaji, mpaliliaji, mvunaji

Mlinzi wa ghala, mjenzi

Shughuli zote zake

Yeye rukwama, lori, punda...

Mwanamke wa Africa

Ni kipi usicho ?

(Tafsiri yetu ; Kiambatisho C)

Hivyo basi wanawake wana jukumu katika harakati za kimazingira katika jamii kwa sababu madhila yanayofanyiwa mazingira hugusa maisha yao ikichukuliwa kwamba makazi ya kinyumbani yamebainishwa kama eneo la mwanamke.

Wanawake hukumbwa na matatizo mengi mazingira na maliasili vinapoharibiwa. Warren (2000:6-12) anajadili matatizo haya hasa anapoangazia takwimu zinazotokana na Shirika la Afya Duniani (WHO) kwamba takriban asilimia 85 ya magonjwa yote yakijumuisha malaria, matatizo yanayotokana na ugonjwa wa kuendesha na hata trachoma katika mataifa ya ulimwengu wa tatu hutokana na kutokuwepo kwa maji safi na kwamba vifo milioni 25 husababishwa na ukosefu wa maji safi ya kunywa na idadi kubwa ya watoto inaweza kuokolewa ikiwa kutakuwepo maji safi

ya kunywa. Ukosefu wa maji ni swala linalofaa kushughulikiwa ipasavyo ili watoto na wanawake wafaidike. Kikundi hiki ndicho kinachohusika zaidi na utekaji maji na wakati ambapo maliasili inaharibiwa au inaangamizwa, wanawake wanalazimika kutembea masafa marefu kusaka bidhaa hii yenye thamani kwao.

Tatizo lingine ni kuwa, maji yanapochafuliwa kutokana na kuvuja kwa kemikali hatari kwenye chemichemi za maji wanaathirika pakubwa. Kiwango kingi zaidi cha maji (mafuriko) na kiwango cha chini zaidi cha maji (ukame) huathiri wanawake. Hali hii hutokana na uzorotaji wa mazingira na matumizi mabaya ya mashamba huku idadi ya watu ikizidi kuongezeka hasa miongoni mwa tabaka maskini. Warren anatolea sababu tatu kuu ambazo zinaleta majanga yanayowaathiri wanawake na si kwamba wanawake pekee ndio wanaathirika bali wanaume wanaathirika ila athari kubwa zaidi huhisiwa na wanawake.Sababu za ukataji miti, kueneakwa jangwa na mmomonyoko wa udongo. Hali hizi zote hufanya afya za wanawake na watoto kudorora hasa wale walio katika tabaka lisilojiweza.

Wanawake katika mataifa yanayoendelea hutumia muda wao mwingi katika upishi wakitumia kuni na hata choo cha wanyama huku wakivuta moshi wenye sumu hasa wanapopikia katika maeneo yasiyo na hewa safi. Moshi huo huwatatiza kiafya hasa kutokana na kemikali zilizomo na ambazo hupelekea wao kupata matatizo ya kiafya. Wengine wao ambao ni waja wazito kupoteza ujauzito huo. Masuala haya yote anayoyaibua Warren yana ithibati ambayo Merchant (1980) anataja kama uhusiano wa wanawake na mazingira hivi kwamba ardhi ilionekana kama mama mtunzaji na kwamba maumbile asili yaliyoko kwenye mazingira ni wazimu na hayathibitiki hasa tunaposhuhudia mawimbi makali ya bahari yanayoleta hasara na hata ukame unaotatiza wengi.Merchant anasisitiza kuwa ardhi ni kiini cha maisha na kwamba mtu hamwui tu mama, kuchimbua dhahabu ndani yake au kuukatakata mwili wake.Ndiposa Nalunnakkal

(2004:59-60) katika makala 'Towards an Organic Womanism: New Contours of Ecofeminism in India' ananukuu Narada Smriti (1993) anayesema,

> Wanawake wameumbwa kwa minajili ya kuleta kizazi, mwanamke ni kama shamba na mwanamme ni mkulima wa shamba hilo. Ikiwa ardhi ni mwanamke lazima ahisi maumivu kwani ardhi inalimwa na kuchimbwa....

Shiva na Mies (1993:14) wanaona uharibifu unaofanyiwa ardhi na vyote vilivyomo na tisho la kuwepo kwa mitandao ya kinyukilia inayotokana na vita kama jambo ambalo wafeministi wa kiekolojia lazima waliangalie kwa makini. Shiva na Mies wanashikilia kwamba wanawake wa mataifa yanayoendelea wanaopigania uhifadhi wa msingi wao wa maisha, huchukulia ardhi kama kiumbe kinachoishi na kinachowahakikishia wao na viumbe wengine uhai. Hivyo basi jukumu kuu la wanawake ni kwamba lazima wajitokeze kupigania mazingira safi na wawe mstari wa mbele kuhamasisha jamii kuhusu athari za udororaji wa mazingira.

## 1.8 Misingi ya kinadharia

Ufeministi ni tapo linalojiegemeza katika maswala ya wanawake katika jamii kwa kutaka kutetea haki na wanawake kwa kudai kwamba watu wote wake kwa waume wameumbwa sawa hivyo wapewe nafasi sawa katika elimu, kuhubiri, kufunza na kufanya kazi ili kupata pesa za kujikimu. Ajenda ya tapo hili ni kuelewa ukandamizaji na kuonyesha kwamba mwanamke anaweza kufanya lolote kama mume. Wamitila (2003:254-6) anaielezea nadharia hii kama inayojitahidi kufasiri uzoefu na tajriba za wanawake kama zinavyojitokeza katika tanzu mbalimbali na hata kushambulia mitazamo ya kiume kuhusu jinsi wanawake wanapaswa kuhisi, kufikiri na kuitikia

hali mbalimbali za kimaisha. Wamitila kwa kuangazia kitabu cha de Beauvoir cha *The Second Sex* anaeleza kuwa utamaduni anamokulia mwanamke una mchango kumdhalilisha mwanamke na kumfanya aamini kuwa anapaswa kuikabili hali hiyo. Mawazo haya ya kukumbatia mfumo wa kibabedume ndiyo yaliyochangia kuwepo kwa misimamo ya kifeministi ambayo ina mikondo mbalimbali anayoiangalia Wamitila.

Mkondo wa kwanza ni ule unaoongozwa na mwanaharakati Germane Greer (ambaye anapendekeza kuwa wanawake wanapaswa kususia asasi hii inayowakandamiza kwa kutoolewa kwani kwa kuolewa mwanamke anageuzwa kitu cha kumilikiwa na kuwako kwake hufutwa. Mkondo mwingine ambao ni wa Kate Millet (1978) unazishambulia kazi za waandishi ambao wanamsawiri mwanamke kwa njia hasi katika kazi zao mbalimbali ili kuendeleza ubabedume na kwamba mawazo ya Sigmund Freud yanatilia nguvu itikadi hii. Mkondo mwingine wa baadaye ukiongozwa na Toril Moi (1985) unachunguza mitazamo ya uwili katika jamii.Uwili huu unajitokeza kwa kumhusisha mwanamume na sifa chanya huku mwanamke akihusishwa na sifa hasi.

Tapo hili la Ufeministi lina matawi mbalimbali jinsi yanavyojadiliwa na Wamitila (2003:255-6). Tawi la kwanza ni la ufeministi wa kibidhaa ambao kutokana na jamii ya ubepari vipengele vingi vya maisha na kiutamaduni vimeathiriwa na ubidhaaishaji hivi kwamba maandishi ya kifeministi na uzalishaji wa kiutamaduni hufanyika na kutumiwa kwa ununuaji na uuzaji wa bidhaa. Tawi la pili ni la ufeministi huru kulingana na Osoro (2003:12) linajihusisha na kupigania haki na mabadiliko ya jumla katika jamii. Linapigania kumalizika kwa ubaguzi kati ya wanawake na wanaume. Wafuasi wa tawi hili wanapendekeza kutekelezwa kwa mabadiliko kupitia kwa njia ya ushawishi, mwamko wa kitabaka na kupigania kuhusishwa kwa masuala yanayowahusu wanawake katika kila eneo la kimaisha. Ni tawi linalokubali ukweli kwamba mwanamke na

mwanamume lazima washirikiane katika nyanja mbalimbali maishani na kinachohitaji ni kubadilishwa kwa mtazamo wa jamiiili mwanamke aweze kutambuliwa kama binadamu sawa na mwanamume. Tawi lingine ni lile la kiharakati ambalo lina msimamo kuwa wanawake wananyanyaswa na kukandamizwa na wanaume na kwamba pana umuhimu wa kuielewa nguvu hiyo. Pia, kuwa 'kike' ni tokeo la miundo ya kijamii bali sio tofauti kati ya jinsia mbili tofauti.

Tawi la nne ni lile la kisoshalisti lililoathiriwa na mawazo ya Karl Marx na ambalo huweka mkazo mkubwa kwenye ukombozi wa mwanamke. Mojawapo wa jukumu la ufeministi ni kuangazia kazi zilizoandikwa na wanawake ili zisipuziliwe wala kudharauliwa. Kulingana na Moore (2008:287) mtazamo wa kifeministi ulijikita katika masuala ya kisiasa na utambulisho wa wanawake kijamii hata hivyo wimbi la pili ufeministi miaka ya sabini na themanini ni kwamba ufeministi haufai kushughulikia tu wanawake lazima ushughulikie unyanyaswaji na ukandamizaji wote. Anaeleza kuwa ufeministi ulielezewa kupitia mchakato wa maelewano na uelewa wa mahusiano ya unyanyasaji unaotokea katika jamii. Uhakiki mpya wa kiekolojia unaipa tapo la kifeministi mwelekeo mpya ambao unadai kuwa jukumu la wanawake la utunzaji watoto unawapa fursa nzuri ya kutunza sayari pia.

Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni nadharia ya ufeministi wa kiekolojia. Ufeministi wa kiekolojia ni kiwakilishi cha muungano wa dhana mbili : ekolojia na ufeministi. Ekolojia hutazama jinsi mifumo mbalimbali ya kimazingira inavyofanya kazi ili kukidhi maisha na jinsi mifumo hii inavyoharibiwa na kusababisha vifo vya mimea na wanyama. Ufeministi nao ni dhana inayohusisha pakubwa wanawake katika kujua haki zao na jinsi wanawake hawa wanavyoweza kupata nafasi sawa katika ajira. Hulenga kubadilisha jamii iliyoegemea kuume na inayowafanya wanaume kuwatawala wanawake.

Ufeministi wa kiekolojia ni uwanja uliochimbuka miaka ya 1970 na 1980 wakati ambapo nadharia na harakati za kifeministi na kimazingira zilipotagusana (Warren 1997 ; Sturgeon 1997 ; Gaard 1993). Ni uwanja uliokua kutokana na vuguvugu la kijamii la wafeministi, la ekolojia na amani kulingana na Shiva, (1993:13). Kwa mujibu wa Taylor (2005) ufeministi wa kiekolojia ni msamiati uliozinduliwa na Mfaransa Francois D'Eaubonne ambaye ndiye mwasisi wake mwaka wa 1974 kuashiria mwingiliano wa ekolojia na ufeministi katika kitabu chake *Le Feminisme ou la Mort* (Ufeministi au Mauti).Dhana hii ilichimuza baadaye wakati fasihi ya kiekolojia ilishika kasi miaka ya tisini. Grazebrook (2002) aliona dhana hii ya ufeministi wa kiekolojia kama dhana iliyokuwa na vianzo vyake katika utamaduni wa Kifaransa. Anashikilia kuwa mwaka wa 1952 Simone de Beauvoir alitaja kuwa wanawake na ekolojia walionekana kama "wengine" hivi kwamba walionekana duni.

Mwaka wa 1974 Francoise d'Eaubonne alibuni dhana ya 'eco-feminism' kuashiria umuhimu wa wanawake kujaribu kuleta mapinduzi ya kiekolojia na hivyo kutumia dhana ya *Le feminisme ou la mort* yaani ufeministi au mauti kujadili matokeo ya kiwango kikubwa cha watu na kudorora kwa maliasili.Mfaransa huyu aliona kuwa kulikuwa na ongezeko la watu na hivyo maliasili iliharibiwa na wingi wa watu. *Le feminisme la mort* ni tahadhari aliyotoa kwamba binadamu hawawezi kuhimili athari za kiekolojia zinazotokana na mifumo ya kijamii inayoegemea kuume.

Kwa mujibu wa Shiva (1993: 13-14), dhana hii ilipata umaarufu tu katika muktadha wa maandamano mengi yaliyopinga uharibifu wa mazingira uliochochea majanga mengi ya kiekolojia. Ufeministi wa kiekolojia baadaye umepata mashiko na kufaraguliwa na nadharia ya ufeministi hivi kwamba kuna matawi yake mbalimbali kama vile ; ufeministi wa kiekolojiaS kwa mtazamo wa kimaksi, kiharakati, kidhanaishi, kisaikolojiachanganuzi, kijamii, kiusasaleo na kihuru. Mitazamo hii hata hivyo yote inaangalia ni jinsi gani kazi ya kifasihi inavyodadavua

masuala ya ekolojia asilia kwa kuegemea ufeministi. Wahakiki wa mtazamo huu huangalia ni jinsi gani mwanamke anavyosawiriwa katika harakati za utetezi wa ekolojia au uharibifu wake, na ni wanawake wangapi wanaojishughulisha na utunzi wa kiekolojia katika fasihi. Pia huweza kuchambua wanawake katika jamii asilia hasa wale wanaojishughulisha na vuguvugu la ekolojia.

Warren (1997:3-4) anasisitiza kuwa mahitaji ya wanawake kama wasimamizi wa kiuchumi nyumbani mwao ni muhimu kwa njia tatu : wanawake wanategemea miti na misitu zaidi kuliko wanaume na kadri misitu inapozidi kukatwa ndivyo matatizo yao yanapoongezeka. Wakati misitu inapoadimika ndipo chakula na vyombo vinavyotegemea miti huadimika hivyo kuwalazimu wao kutembea kwa umbali kusaka chakula na mahitaji mengine na wakati huohuo wanaume hupotelea mijini kuajiriwa katika kampuni wakiwaacha wanawake na majukumu yao. Baadhi ya mihimili ya nadharia hii ni kama vile:

a) Ukandamizaji wa aina yoyote katika jamii unahusiana na mwingine na hivyo basi mifumo yote ya ukandamizaji lazima ishughulikiwe. Mifumo hii hujikita katika utamaduni duni na utawala mbaya. Mtazamo wa Merchant (1980) ni kuwa ukandamizaji wa mwanamke ni ukandamizaji wa ekolojia ndiposa wanawake wanajihusisha zaidi kuona ekolojia haitawaliwi. Utamaduni unaodunisha mwanamke ni ule ule unaodunisha ekolojia na hivyo ipo haja ya kupinga utamaduni wa aina hii kwa lengo la usawa kijinsia na haki kwa ekolojia na mtandao wa viungauhai.Ndiposa nafasi ya mwanamke katika kujikomboa na kukomboa ekolojia ndiyo mhimili mkuu unaosababisha watunzi wa fasihi na sanaa ya Kiswahili kujitosa katika kazi bunifu zinazomweka mwanamke kama mhusika mkuu.
b) Hakuna uhuru kwa mwanamke na suluhu la matatizo ya ekolojia halitapatikana katika jamii ikiwa watatawaliwa. Lazima wanawake waunganishe matakwa yao na yale ya

ekolojia. Haiwezekani kutatua umaskini na ukandamizaji wa mwanamke pasipo kumkabidhi uwezo; uwezo wa kurejesha mfumo wa ekolojia kupitia kwa utunzaji mazingira

c) Mifumo ya kijamii huwabainisha wanawake kama watunzaji watoto na wanajamii wengine wasiojiweza, yaya na ni wafanyikazi wanaopewa ujira mdogo. Jinsi mwanamke alivyo mpaji wa uhai ndivyo ardhi na maumbile asilia yalivyo basi pana haja ya kutunza kile kilicho na uhai wa mwanadamu.

d) Mifumo ya kijamii na kisiasa huleta madhara makubwa katika mazingira hivyo basi wanawake kwa njia moja au nyingine hupitia matatizo ya kimazingira inayogusa maisha yao na hivyo wana nafasi nzuri ya kutetea ekolojia isiharibiwe.

e) Teknolojia za kisasa zimeleta athari kwa mazingira hivyo pana haja ya kulindwa kwa mazingira ili mikasa inayowaathiri zaidi wanawake isiongezeke.

f) Utawala wa kibabedume ndio mfumo unaozalisha ukandamizaji wa aina hii katika jamii zetu jinsi anayojadili Taylor (2005:533-534). Watetezi wa nadharia hii wanadai kwamba mifumo ya kibabedume inajikita katika falsafa ya uwili (dualism) inayobainisha mwili/roho, kike/kiume, mwanadamu/mnyama na utamaduni/mazingira. Ikiwa falsafa hii itazidi kutawala, basi haitawezekana kukomboa mwanamke na ekolojia inayokandamizwa. Mitazamo hii ya kifalsafa lazima idenguliwe na kufanya jamii kuwa moja katika kila hali; kwa jinsi hii basi mwanadamu anaweza akafaulu kukomboa ekolojia yake na pia elementi nyinginezo zinazokandamizwa.

Wanaekolojia kifeministi kama vile Susan Griffin (1978), Vandana Shiva (1988), Sallie McFague (1993), Greta Gaard (1993), Ruether (1996), Karen Warren (1997) Ivone Gebara (1999), walijitokeza na kudai kwamba ukandamizaji wa aina yoyote katika jamii unafungamana

na mifumo yote ya kijamii na ili kutatua shida hii, lazima ishughulikiwe kwa ukamilifu.Ukandamizaji wa wanawake na mazingira ni dhana mbili ambazo hazina budi kutanzuliwa kwa pamoja. Kaul Dagny (1997:102) katika makala yake amebaini kuna uhusiano kati ya kudorora kwa ekolojia na ubaguzi dhidi ya wanawake hivyo basi ufeministi wa kiekolojia lazima uweze kuleta maelewano mapya ya ekolojia. Dhana hii inashikilia msimamo kuwa wanawake wana ukaribu mno na ekolojia kwani ni wapaji wa uhai watunzaji wa uhai na pia mbegu ya uhai huchimuza ndani mwao. Nadharia hii inaweka umuhimu wa utunzaji wa ekolojia ili uhai wa kizazi kisipotee na kiweze kufaidi rasilmali asili zilizoko kwenye mazingira ya mwanadamu.

### 1.8.1 Upungufu wa nadharia

Hata ingawa nadharia hii inaweka mbele maswala ya mahusiko ya wanawake katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira, mjadala huu unakosa kutilia maanani juhudi za vikundi vingine katika jamii. Hali ya kutenga mchango wa wanaume katika vipengele vya nadharia hii, ni kama kuishi katika maisha baguzi ambayo yanawaona wanaume kama adui wa wanawake na kwamba ndicho chanzo cha kuteseka kwa wanawake. Hali ya kuwepo kwa mjadala tengaji ni upungufu mkubwa unaozuka katika nadharia hii na ambao hauwasilishi hali halisia ya sasa hasa ikichukuliwa kwamba matatizo ya kimazingira yana athari kwa kila mwanajamii; wa kike au kiume.

Utatumiaji nadharia hii kama inaupungufu??

## 1.9 Mbinu za utafiti

Utafiti huu ulifuata muundo wa uchanganuzi wa makala ambapo maelezo yetu yaliangazia masuala tata yaliyoko kwenye matini tuele. Muda mwingi wa utafiti huu ulikuwa kupitia maandishi kwenye maktaba na kuepuka swala la nyanjani kwa madhumuni ya ukusanyaji data. Tulizingatia riwaya ya Clara Momanyi ya *Nakuruto* kwani riwaya nyingi zilizochapishwa hazijamulika swala la mchango wa wanawake katika uhifadhi wa mazingira. Pia, riwaya hii ni mojawapo wa riwaya za kisasa ambazo zinayapa masuala ibuka kipaumbele.

Utafiti wetu ulikita katika kuchanganua riwaya ya kimazingira. Kulingana na lengo la utafiti wetu kazi nzima ilisomwa na aya husika zinazotaja hoja moja kwa moja zilinukuliwa.Data ya kimsingi ilitokana na riwaya teule ya *Nakuruto*. Kutokana umilisi wa mtafiti katika maswala ya kimazingira, sentenzi zenye hoja zilizokuwa muhimu kwenye uchanganuzi wa mazingira katika kazi teule ziliwekwa bayana.

Kwa upande mwingine, data ya kijumla ilipatikana katika majarida na vitabu mbalimbali. Vitabu vilivyotumika kuliweka bayana swala la ufeministi wa kiekolojia ni vile vinavyojadili masuala ya ekolojia na kuzingatia misimamo ya kifeministi. Tulihusisha pakubwa mtandao kwani maswala ya kimazingira yametolewa mchango kwenye majarida ambayo usambazaji wake mwingi ni kupitia kwenye mtandao. Data hii ilikuwa muhimu kwani iliweka msingi wa uchanganuzi wa data yetu ya kimsingi pia ilikuwa muhimu kwa kuchora picha halisi ya mazingira na kumpa mtafiti mwelekeo wa kimazingira. Matini teule ilichanganuliwa kwa kuihusisha na mihimili ya nadharia ya ufeministi wa kiekolojia.

# SURA YA PILI

# SWALA LA KIMAZINGIRA KATIKA FASIHI ANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Katika sehemu hii, fasihi andishi zinazoangazia uharibifu wa mazingira zilichunguzwa. Baadhi ya vitabu vinavyomulika swala hili vilielezewa ingawa kwa muhtasari ili maelewano yawepo kwamba dhima ya uharibifu wa mazingira na utatuzi wake ni mambo ambayo watunzi tayari walitilia maanani hata kabla ya karne ya ishirini na moja. Muhtasari wa riwaya teule ya *Nakuruto* umetolewa ili kuwepo na uelewa wa kazi iliyojadiliwa na kumpa mwanga yeyote atakayeitalii kazi hii.

## 2.2 Tungo za kimazingira

Kazi za kimazingira zimechipuka kuangazia swala la kimazingira katika riwaya, tamthilia na hata ushairi. Fasihi ya Kiswahili imeweza kulijadili swala la kimazingira kupitia watunzi wa mashairi tamthilia nariwaya.Mashairi ya mwanzoni yalitokea kwenye mkusanyiko wa mashairi ya Kezilahabi (1974) katika diwani yake *Kichomi.* Shairi la "Uvuaji wa Samaki Victoria" ni mojawapo ya shairi linaloelezea ulafi uliojiri miongoni mwa wavuaji hivi kwamba wanavua kupita kiwango kinachostahili hivyo basi pana haja ya kuangalia upya kazi hii ya uvuaji ambayo imebadilishwa na kuwa kama kitega uchumi.

Katika mikusanyiko ya mashairi mbalimbali watunzi wameshughulikia mada mbalimbali na kuingiza mada za kimazingira katika baadhi ya tungo zao. Katika mkusanyiko wa mashairi ya *Jicho la Ndani* ya Mohamed (2001) Shairi la "Ndege Wamekufa" (uk.110) linaashiria kiwango

kilichofikiwa kutokana na uharibifu wa mazingira ambao hasara zake zina ithibati isiyoweza kufichika kamwe. Ndege wa aina aina; chiriku, tausi, mramba, kasuku na hata kuku tumewapoteza ndiposa mtunzi alitunga shairi la kusifia ardhi ambayo ni uhai wake (uk.44) kwamba ardhi ni uhai wake.

Mkusanyiko wa mashairi yaliyomo katika *Bara Jingine* (2001), mtunzi Mberia anaangazia matendo ya kibinadamu yanayoleta maafa kwenye mazingira. Mtunzi anasimulia aliyoyaona katika ndoto kwenye shairi la "Jinamizi" kuwa, kaumu ya watu inavyonyonga chemichemi kupitia kwa misumeno, shoka na panga kali. Shairi la "Ngao" (uk.59) Mberia anawasilisha uharibifu unaotendwa na kuumiza ozoni kupitia kemikali jeuri ingawa ozoni hii ni ngao ya uhai wetu ambao unalindwa kutokana na tumbo la jua kutokana na mauti. Matendo ya kibinadamu ya uharibifu yanadhihirika katika shairi la "Mimi, Mto Nairobi" na "Bwawa la Ithanje" ambapo uchafu wa viwanda na kemikali unaelekezwa kwenye chemichemi za maji.

Vilevile mwelekeo wa mtunzi Mberia katika *Redio na Mwezi* baadhi ya mashairi ni kwamba, tatizo la kimazingira lipo na lazima utunzi wa fasihi uweze kuweka wazi maswala haya.Mtunzi wake ambaye anamulika mazingira katika shairi la 'Johari La Bamburi' katika *Redio na Mwezi* lakini wakati huu anaonyesha jinsi chimbo lilivyobadilika hivi kwamba mfumo wa ekolojia umebadilika na kuwa eneo la watalii eneo la Mombasa.

Katika tamthilia, kazi ya Bwana Elias K.Maarugu ya *Adui wa Umma* (1992) ni mchezo ambao ni tafsiri ya mchezo wa Ibsen wa *An Enemy of the people* (1882) unaoangazia tatizo la kimazingira linalotokana na ubinafsi wa viongozi.Viongozi wamejawa na tabia ya uroho na ubinafsi hivi kwamba mipango waliyo nayo ya kuleta mapato katika manispaa inakubwa na utata hivi

kwamba maji yanayowafaidi watalii na watumiaji wa hamumu yanachafuliwa kutokana na kiwanda cha ngozi kinachomilikiwa na Morten Kiil. Katika mchezo huu Dkt. Stockmann anasimama kidete kutetea utafiti wake uliong'amua kuwa chanzo cha maradhi yaliyokuwa yakisumbua watalii ni maji yaliyochafuliwa. Meya ambaye hakubaliani na uvumbuzi wa nduguye na kuona kuwa marekebisho aliyoyataja Dkt. Stockmann yatagharimu manispaa hela nyingi, anaufanya umma wote umchukie Dkt. Stockmann anayebaki kuungwa mkono na familia yake. Bwana Mortein Kiil ni bwenyenye aliyewekeza pakubwa kwenye kiwanda hayuko tayari kuunga mkono ripoti hiyo kwani kuunga mkono kwake kutamaanisha kiwanda kifungwe. Hali ya kutaka kuwaficha mabwenyenye na kutochukua hatua ndiyo inayopelekea uharibifu mkubwa wa mazingira. Mabwenyenye kama Kiil ndiyo wanaomiliki majengo makubwa hata ufukweni na ambao wanajali maslahi yao bila kuangazia madhara kwa mazingira. Ingawa mchezo huu ulitungwa zaidi ya miaka 100, una manufaa katika mazingira ya sasa na hata baadaye.

Tamthilia yake Kithaka wa Mberia ya *Kifo Kisimani* (2001) inachangia kwa kuangazia jinsi ambavyo utawala mbaya unavyoweza kuchangia katika uharibifu wa mazingira. Mtemi Bokono na utawala wake wanakwenda kinyume na matumizi ya maliasili hivi kwamba chemichemi zilizopo za maji ni mali ya watu wake wenyeji wamenyimwa fursa ya kufaidika kutokana na maliasili hizi. Ugawaji wa ardhi hata isiyostahili unafanyika hasa wakati kiwanja cha kuchezea watoto kinaponyakuliwa. Pia tunaona ahadi anayopewa Gege kuwa atapewa ardhi nzuri (uk.31) na katika kufanya hivi, uongozi unajaribu kunyamazisha wapinzani wake. Swala la uzorotaji wa mazingira limemulikwa hasa kupitia kwa mhusika Mwelusi hasa anaposema kuwa dhiki zao zimesababishwa na utawala mbaya ambao umekausha chemichemi za maji zilizoleta uhai waq wanabutangi wote (uk.45). Anachokiwakilisha mtunzi Wa Mberia ni kuwa utawala una uhusiano mkubwa na aidha uzorotaji wa mazingira au uhifadhi wa mazingira.

Katika utanzu wa riwaya, Mbogo (2002) katika *Bustani ya Edeni* anayamulika maswala ya kimazingira kwa uwazi kabisa mandhari ya riwaya hiyo yakiwa pwani ya Tanzania mji wa Dar es Salaam. Riwaya hii inaangazia matatizo yanayosababishwa na kiwanda cha kemikali kinachojulikana kama Sagasaga kinachoendeleza uchafuzi wa hewa kwa kuelekeza taka zake kwenye mto Zamala.Wafanyikazi wake wanatatizika na magonjwa huku mimea na wanyama wakiaga kutokana na maji yenye sumu. Riwaya hii inaweka bayana matatizo ya kimazingira yanayotokana na matendo ya kibinadamu katika fasihi ya Kiswahili

## 2.3 Muhtasari wa riwaya ya *Nakuruto*

Riwaya ya *Nakuruto* ni moja ya riwaya kadhaa na tungo zingine za Kiswahili zinazolenga kuzindua ung'amuzi wa kijamii kuhusu suala la ekolojia na mabadiliko ya angahewa. Riwaya hii imetungwa katika masumulizi ya ndoto huku mhusika mkuu akiwa ni mwanamke anayeitwa Nakuruto. Mtunzi anamtumia mhusika mkuu Nakuruto kama chagizo cha kuleta mabadiliko ya kiekolojia na tabianchi kwa faida ya mustakabali wa jamii.

Nakuruto anabebwa na nguvu za kimazingaombwe na kupelekwa katika sehemu mbalimbali na nyakati tofautitofauti za ukuaji wake. Kwanza mtunzi anambeba Nakuruto hadi katika dunia ya kale, katika enzi ya mwanzo wa maisha ya 'zamadamu' ambapo wanadamu, wanyama na viumbe wengine walikuwa wanaishi kwa utangamano. Wakati huu ndio binadamu alikuwa anabadilika kimaumbile, anaishi mapangoni, na chakula chake hakiathiri uhai wa mazingira. Nakuruto anapitishwa katika mapango yaliyojaa vitu ajabuajabu na kuuona uhalisi wa kale. Katika baadhi ya mapango mwanga mkali unajibainisha katika milima mirefu iliyotiririsha vijito

kwenye msitu uliosheheni viumbe wa kila aina. Baadaye, nguvu hizi zinamwachilia kwenye jangwa lisilo na uhai wowote.

Baadaye nguvu za kimazingaombwe zinamsomba na kumrusha katika dunia ambapo mahusiano mema baina ya mwanadamu na viumbe wengine yamedorora hivyo kuzalisha uhasama.Binadamu anawinda wanyama kwa zana mbalimbali na yeye yuko tayari kujikinga dhidi ya uvamizi wowote. Huu ni wakati ambapo mahusiano mema ya binadamu na wanyama yamo hatarini kwa sababu za kujikimu kimaisha.

Kadiri Nakuruto anavyopeperushwa katika historia mbalimbali za maisha yake, ndivyo anavyotambua jinsi binadamu alivyohasiri mifumo ya mtandao wa viungauhai. Mito iliyokuwa mizuri na safi imechafuliwa na kukauka, miti ya kiasili iliyokuwa inawanda imekatwa, na mitandao yote ya kiekolojia imedhoofika kiasi cha kusababisha njaa, ukame na matatizo kwa viumbe wote. Anashuhudia uchafuzi wa aina aina kwenye ziwa katika na wenyeji wa kijiji cha Latimbi ambao wamesababisha kushuka kwa viwango vya maji katika mto Milu.

Kijiji cha Maweni kimekumbwa na ulitima ambao umesababishwa na wachache wanaomiliki sehemu za rutuba. Mabwanyenye hawa wengi ni wazungu kutoka Ulaya na hawajali hali ya maskini ambao ni wengi. Wanafuja mali na rasilimali ya wananchi huku wananchi wakibaki katika lindi la umaskini na kuishi maisha ya kutegemea wengine. Maskini hawa ambao ni wachache wamebakia kwenye sehemu zisizozalisha chochote huku wakikalia kwenye mazingira yaliyojaa rundiko la taka na majeshi ya panya.Katika kijiji cha Maboni hali sio tofauti na vijiji vingine kwani uharibifu wa mazingira unashuhudiwa.

Nakuruto anatumiwa na nguvu hizi za kimazingaombwe kuzindua jamii ya wanadamu kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira kwa ajili yao wenyewe na viumbe wengine katika sayari. Kani katika ung'amuzi wa mhusika huyu mkuu zinasukumwa na kile ambacho anashuhudia katika kila kadhia anayopelekwa ndotoni.Licha ya kuwepo kwa pingamizi na changamoto nyingi kuhusiana na juhudi zake, Nakuruto anafanikiwa kubadilisha tabia ya nchi kwa kushirikiana na wenyeji kuondoa visababishi vya uharibifu hivyo kukomboa nchi yake ya ndoto kutokana na athari za uharibifu wa ekolojia.

## 2.4 Hitimisho

Sehemu hii imeangazia baadhi ya tungo za kifasihi zilizo na mielekeo ya kimazingira. Hivi si kusema kuwa hizi ndizo tungo pekee zinazopatikana katika fasihi ya Kiswahili bali ni kuweka bayana wazo kuwa ni baadhi ya tungo ambazo zimechangia katika kuelezea uovu unaotendewa mazingira yetu. Ufupisho wa riwaya ya *Nakuruto* umewasilisha mwelekeo mpya wa kijinsia katika swala hili kwamba, tofauti na kusimulia moja kwa moja kuhusu sehemu ya wanawake katika jamii, mtunzi anamhusisha mwanamke katika kupigania mazingira kwa manufaa ya kizazi kijacho. Watunzi wa fasihi wameweza kuwasilisha kazi zao kiubunifu kwa njia ya uumbaji wa madhari yanayolenga sehemu fulani kimazingira ndiposa tunapata fasihi hasa riwaya za visiwani na zile za bara kutokana na masimulizi ya kimazingira. Utunzi huu unatilia maanani kwamba mandhariyana athari fulani katika usimulizi au usomaji wa fasihi unamfanya msomajiyeyote kung'amua kuwa mazingira yetu yana umuhimu mkubwa na yanatoa mchango katika ubunifu wetu.

# SURA YA TATU

## MCHANGO WA UFEMINISTI WA KIEKOLOJIA

### 3.1 Utangulizi

Sehemu hii imeangazia uchanganuzi wa riwaya ya *Nakuruto* kulingana na madhumuni ya utafiti kwa kuongozwa na maswali ya utafiti. Mchango wa fasihi ya kiekolojia umejadiliwa kwa kuzingatia elimu kwa, pingamizi katika uhifadhi mazingira na matatizo yanayokumba wanawake katika riwaya hii.

### 3.2 Fasihi ya ufeministi wa kiekolojia

Mtunzi alitunga riwaya ya *Nakuruto* kwa kuzingatia masuala ya ekolojia ambayo anayahusisha na mwanamke anayewakilishwa na mhusika mkuu Nakuruto. Masuala haya lazima apigane nayo ili ulimwengu wake uboreshwe. Katika kufikia uhifadhi kamili wa kimazingira lazima mwanamke kama mlinzi wa mazingira aweze kujitokeza ili ahamasishe jamii kuhusu hatari zilizo mbeleni ikiwa mazingira yatadorora.Katika kujitokeza kwake lazima awape wananchi elimu mwafaka, aongoze shughuli za ukumboaji wa mazingira na ahusike katika kuondoa asasi zinazorudisha nyuma uhifadhi. Kaul Dagny (1997:102) anaibuka na mjadala kuwa pana haja ya ufeministi wa kiekolojia kuleta maelewano mapya ya kiekolojia. Dhana hii inashikilia msimamo kuwa wanawake wana ukaribu mno na ekolojia kwani ni wapaji wa uhai watunzaji wa uhai na pia mbegu ya uhai huchimuza ndani mwao. Hali hii inamfanya mwanamke kuwa kiumbe bora atakayehisi uchungu mazingira yake yanapodorora na pia ndiye atakayefurahikia pakubwa ikiwa

njia mwafaka za utunzaji zitakapowekwa ili kulinda uhai huu muhimu. Hivyo basi, mchango wa ufeministi wa kiekolojia ni kuwazindua wanajamii hasa wanawake wapiganie utunzaji wa mazingira yao. Kupitia uzinduzi huu, wataweza kuyakomboa mazingira yao na kurejesha uhai mpya katika jamii.

### 3.2.1 Uzinduzi

Uhusiano mkubwa upo hasa unapochunguza ukosefu wa miti na kukauka kwa vyanzi vya maji. Kila tone la mvua linaloanguka linapenyeza ardhini hadi kwenye vihifadhi vya maji vilivyo chini ya ardhi, na hivi ndivyo hupatia vyanzi vilivyoko kwenye uso wa dunia maji kila wakati. Wanavijiji wa Latimbi, Machinjioni, Maboni, hawakufahamu uhusiano huu wa kiekolojia hadi Nakuruto alipowazindua. Wanajamii hawa hawakujua kiasi gani wanavyotegemea mfumo wa ekolojia ndiposa wanakata miti na kuharibu maeneo oevu kwa manufaa ya kiuchumi. Katika kila kijiji anawazindua wanajamii wote bila kujali jinsia kwa lengo la kurejesha mfumo wa ekolojia kwa upanzi wa miti, kuondoa wanyonyaji wa ardhi na sera zao kandamizi. Nakuruto anapofikia ukingoni mwa ziwa Ipe na kugundua hatari iliyokuwa ikichungulia wanakijiji kwa kuharibu mazingira ya ziwa, anawazindua ili wafahamu kwamba lazima walinde ziwa hili. Anawauliza,

> Chanzo cha mwendelezo wa uhai wenu ni Ipe, nanyi mko mbioni kuukatiza. Je, mtoto mchanga akikatiziwa ziwa la mamaye hatotishiwa uhai wake? Fikiria jibu la swali hili (uk.32)

Katika dondoo hili ni wazi kuwa wanajamii hawakuwa na maarifa yoyote kuhusu kile kinachositiri uhai wao ndiposa wanaendeleza uharibifu kwenye ziwa. Nakuruto hasitishwi bali anaendelea kutoa tahadhari na hata kuwasihi kupitisha ujumbe na kuibuka na mikakati ya

kutunza ziwa. Uzinduzi wake hauambulii patupu kwani hata mama Bintifundi (36) anakubaliana na yale aliyonena Nakuruto.

Nakuruto anajitokeza kama mkufunzi kwenye masuala ya kimazingira kila apitapo kijiji hata kijiji. Jinsi ambavyo mwanamke anavyohimili uhai wa wanawe ndivyo ambavyo elementi za kimazingira zinavyohimili uhai wa wanadamu. Analinganisha elementi za kimazingira na uhai wa mwanadamu kwa kusema kuwa,

> Maji pumzi ya uhai.Ardhi kitovu cha uhai. Ni furaha iliyoje maji yanapobusu ardhi na kuchipua uhai (uk.28) Ole wako ewe mzazi unayepokwa uwezo wako wa kuendeleza kizazi (uk.105).

Nakuruto anajawa na simanzi kunapotokea mashindano ya kusaka kujitajirisha kiasi cha kuhasiri sayari. Alihisi kwamba,

> Uharibifu wa mali asili katika sakata ya kuimiliki nta ulielekea kuitia sayari waliyotunikiwa na Muumba wao uyabisi ishindwe kuzalisha na kuhimili uhai wa viumbe (uk.101)

Usemi wake kwa Ludao anayechimba mitaro kupitisha maji ya ziwa shambani mwake unapasha habari muhimu kuhusu sababu zinazochangia kukauka kwa vianzi vya maji. Anasema,

> Mitaro mingi mnayochimba mahali hapa mtakuja kukausha Ipe Ludao...Chanzo cha uhai wenu ni Ipe, nanyi mko mbioni kuukatiza (uk.32).
>
> Wanadamu tumetunukiwa zawadi za kudumu na Muumba lakini tunazitumia vibaya kwa hasara yetu wenyewe. Tunasafisha nyumba zetu kila siku.Miili yetu tunaisafisha kila uchao, lakini hatujali kupasafisha mahali panapositiri uhai wetu.

Ole wetu tunajikaanga kwa mafuta yetu wenyewe (uk.34) na kwamba "hasara humfika mwenye mabezo. Tusipopunguza uchafuzi huu, maisha yetu yamo hatarini (uk.35).

Wito wa Nakuruto kwa wanakijiji umeshabihiana na wito wa makamu wa rais nchini Tanzania katika uzinduzi wa mradi wa maji na usafi wa mazingira katika manispaa ya Songea aliposema, "Mnapoelezwa msilime kwenye vyanzo vya maji mkubali, na wala msichukie kwani mkikaidi mtaharibu vyanzo hivyo na kuathiri upatikanaji wa maji... Dunia nzima hivi sasa imetaharuki, kuna mabadiliko ya tabianchi ; hali ya hewa na miongo imebadilika, mvua hazijui msimu tena. Tuyatunze mazingira yatutunze na Ruvuma iendelee kuwa kijana" (Ameir, 2010:3-4).

Vile vile Nakuruto anapozindua kijiji cha Walatimbi kuhusu kujikomboa, wengi wanamkataa ingawa hatimaye wanakubali itikadi yake ya kukomboa kijiji chao na kurudisha hali halisi ya maisha yao kama ilivyokuwa siku za awali. Mkude wa Magonji ambaye ni mmoja wa wahusika katika shamba la Bwana Brook anadai kwamba,

> Ikiwa huishi hapa, dhiki yetu utaifahamu vipi hata ukielezwa ? Bibie, usinipotezee wakati wangu bure. Sina wasaa wa kusukuma soga hapa...
>
> Ni kweli anayosema Mkude, mie sina hata maji mwangu nyumbani, achilia mbali chakula.Nawe, wataka tuzungumze.Bi.Mkubwa, huna watoto wanaokusubiri nyumbani? Mama mmoja alimuuliza Nakuruto. (uk.41).

### 3.2.2 Ukombozi

Ukombozi wa mazingira ni juhudi zinazofanywa kuhakikisha kwamba uharibifu unaotendewa mazingira na maliasili umepunguzwa au hata kukomeshwa ili mwanadamu aweze kufurahikia ekolojia yake. Katika riwaya ya *Nakuruto*, mhusika Nakuruto ameweza kusimama kidete kupigania ukombozi wa mazingira kupitia kwa ushirikiano wake na wanavijiji mbalimbali. Shiva na Mies (1993:15) wanaeleza kuwa wanawake waliokuwa mstari wa mbele katika maandamano yaliyokuwa yakipinga ujenzi wa kiwanda cha nguvu za kinyuklia eneo la Whyl Kusini magharibi mwa Ujerumani wote hawakuwa wafeministi bali ni wale walioona kuwa teknolojia ingeathiri kizazi kijacho na kuzingatia kwamba kulikuweko na uhusiano kati ya teknolojia, uimarikaji wa viwanda na unyonyaji wa mataifa ya ulimwengu wa tatu. Ukombozi ni dhana ambayo wanawake katika maandamano ya Chipko eneo la Himalayas walilikumbatia ili kuhifadhi spishi mbalimbali za miti.Wito wa ukombozi unatumiwa na Nakuruto anapopanga kumwondoa bwana Brook katika mashamba ya Walatimbi ili kukomboa ardhi yao. Anashauri umati ulivamwie kasri na hata kulitia moto ili Bw. Brook asipate nafasi ya kurudi tena. Katika kumwondoa mnyonyaji huyu wataweza kukomboa mashamba yao na kuimarisha hali ya shibe majumbani mwao jinsi asemavyo Nakuruto:

> Mkishafaulu kumwondoa haini yule katika ardhi yenu, jigawanyieni mashamba ambayo ni haki yenu mliyorithi kutoka kwa mababu zenu. Kuzeni mazao ya kila aina mlishe wana wenu.Bila kukita mizizi sawsawa katika ardhi yenye rutuba, makuunge na matagaa hunyauka na uhai kupotea. Fahamuni hili... (Uk.44- 45).

Mzee Saluda anamweleza Nakuruto yanayokumba kijiji cha Maweni kwamba wazungu wenye asili tofauti ndio wanaofuga mifugo wengi na kulima mashamba jinsi wapendavyo mwishowe bidhaa husafirishwa kwao hivyo wanakijiji wameishia kutofaidika na kuwepo kwa wazungu

hao.Nakuruto anamweleza Mfumwa mpango wake wa kumwondoa Wellingtone ambao anautaja kama 'wokovu'

> ...Hayatakuwa maangamizi bali wokovu kutoka katika silisili za hasidi yule... (uk.65)

Mwishowe, mpango huu unafaulu wazungu wanapohama na kufunga kiwanda na maisha mapya kuanza kupitia kwa ushauri wake Nakuruto kwamba,

> Nawashauri kuwa kazi ya kuchimba visima ianze himaujuzi wa kuchimba ardhi mnao, kwa hivyo eneo hili litapakae visima na mabwawa ya maji. Tumieni maji haya kwa ukulima na ufugaji wa wanyama. Mashamba na bustani zenu zitanawiri ka wingi wa rasilimali hii. Miti itamea na misitu itachipuka na kusitiri maji... (Uk.71).

Ukombozi ndiyo mbinu ambayo mhusika mkuu Nakuruto anatumia ili kuleta mabadiliko ya kimazingira. Anawakusanya maskini katika tabaka la chini kisha kuwachochea kubadilisha hali yao. Juhudi za Nakuruto kama mwanajamii wa kawaida asiyekuwa na lolote isipokuwa ndoto ya mabadiliko ndiyo inayosababisha wanajamii kupindua utawala dhalimu na wa kimaslahi kwa ajili ya mazingira yao, mustakabali wao na watoto wao. Kila mara Nakuruto ameongoza mapinduzi, jamii imeishia kujiweka katika ubora wa maisha kama ilivyokuwa siku za mababu zao (uk. 42-50; 66-73). Kila mwanajamii mwenye maono na uongozi anastahili kuzindua jamii yake bila uoga wowote.

### 3.2.3 Matatizo ya wanawake

Endapo tatizo la kimazingira litatokea basi wanawake hawana budi kubeba mzigo huo mkubwa tofauti na wenzao wa kiume. Mawazo haya ndiyo anayoyajadili Warren (2000:8-10) na kuongeza kuwa idadi kubwa ya watu ulimwenguni huishi katika hali maskini huku wengi wao wakiwa wanawake na watoto. Wanawake hawa hupata mapato ya chini, muda wao mwingi hutumika katika kufanya kazi huku wakimiliki kiasi cha chini zaidi cha mali ikilinganishwa na wenzao wa kiume. Vilevile, ni wasimamizi wa mashamba na maamuzi muhimu ya mazao hutolewa nao.

Wanawake humu nchini hasa wale wa vijijini wanategemea zaidi maliasili hasa maji ya mito, visima na ziwa kwa matumizi ya nyumbani. Upishi unategemea pakubwa kuni kutoka misituni na maeneo yenye miti. Kilimo chao ni cha kiwango kidogo ambacho idadi ya wanawake inayohusika ni kubwa ikilinganishwa na idadi ya wanaume wanaopendelea ujira mwingine. Shiva (1988:119) anaimulika jamii moja ya Kallas ya India iliyo na tofauti kubwa katika sekta ya ajira kwa wanawake na wanaume. Katika jamii hii, ujira wanaopata wanaume ni maradufu ukilinganishwa na wanawake huku wanawake wakiwa ndio wanaostahili kutoa mahari. Wanawake hawa wanalazimika kujiingiza katika harakati za kulinda mazingira iliwasipoteze fedha nyingi iwapo maliasili itaharibiwa.

Kupitia usimulizi wa Nakuruto tunakumbana na matatizo yanayokumba wanavijiji wakati ukame unaposhuhudiwa nchini. Anasema,

> ...Kwa muda mrefu mvua haikunyesha na watu wakataabika sana. Wengine hata walikufa njaa kwani chakula kiliadimika kabisa. Akina mama wachanga kama wewe waliteleka vyungu wakachemsha mawe mjukuu wangu ili kuwaaminisha

watoto kuwa chakula kiko mekoni. Watoto walisubiri chakula kiive hadi wakalala kando ya meko.... (uk.18)

Hali hii ya kushuhudiwa kwa ukame ndiyo inayompa Nakuruto changamoto ya kuleta mabadiliko hasa anapokariri kuwa,

> Maji yabubujikayo kutoka katika chemichemi zile ndiyo yanayositiri uhai wa viumbe wale. Maji yanaleta uhai kama vile mama mzazi anavyoendeleza uhai wa mwanawe kupitia bubujiko la maziwa yake. Naam mimi ndiye niliyekirimiwa uwezo wa kuendeleza kizazi cha binadamu. Ndimi chanzo cha rutuba nichipuzaye miche ya wana na kufaidi vizazi na vizazi. Bila mimi hakuna uhai wa kizazi cha binadamu. *Kama ardhi, ninahimili maisha ya wengi kupitia uhai wa pumzi yangu,* mapigo ya damu mishipani mwangu na michirizi ya jasho langu. (uk.51)

Usemi huu unaafikaiana na mawazo ya Dagny (1997) ya kuwa, wanawake ni wapaji uhai, watunzaji uhai na mbegu za uhai huchimuza kupitia kwao. Kwa kuelewa dhana hii, mhusika Nakuruto anajaribu kuhifadhi mazingira ili kizazi cha kesho kisipitie matatizo yaliyoko sasa.

Ikiwa wanawake wataelewa jukumu lao katika utunzaji mazingira majanga yanayowakumba yatamalizika. Ripoti ya UNDP (2005) inayojadili maendeleo ya mwanadamu inaelezea kuwa, kutokuwa na usawa wa kijinsia kunaleta ukosefu wa usawa katika mataifa yaliyoendelea na yale yasiyoendelea huku wengi wa watu wanaoishi katika lindi la umaskini wakiwa wanawake. Wanawake na wasichana wanao mzigo mzito unaotokana na uharibifu wa mazingira hivyo wanayo majukumu sawa ya kulinda mazingira. Wanaume nao hawajaachwa nyuma katka kutetea mazingira ndiposa wahusika kama vile; Mzee Saluda, Ludao, Mkude, Bw.Mfumwa, Leboni, Ba. Chande, Mzee Ngocho, Ba. Mrisho na wengine ingawa walipinga juhudi za Nakuruto,

mwishowe wanashirikiana naye katika kuwaondoa wafujaji wa maliasili yao. Hivyo basi, kwa kila mwanajamii kuelewa nafasi yao katika jamii na uhusiano wao na mazingira tunaelekea katika upataji na uimarishaji wa maendeleo.

Katika kijiji cha Latimbi wake kwa waume ni vibarua waliokuwa wakihudumia shamba la pamba. Mzigo walio nao ni mkubwa kando na kukosa mastakimu mazuri wanatumikishwa na bwenyenye aliyenyakua ardhi na kuwanyima walatimbi faida ya mto Milu. Tunasimuliwa kwamba,

> Nakuruto aliweza kuona vibarua kwa mbali wakihudumia shamba hilo ambalo lilipandwa pamba. Wengine walikuwa wakivuna pamba na wengine wakishindilia kwenye magunia. Aliwaona akina mama wakiwa na watoto migongoni wakijitwika magunia hayo na kuelekea kwenye kinu kikubwa cha kuchambulia pamba. (uk.37).Nakuruto aliwatazama kwa huzuni akina mama waliodhoofika wakichuma pamba juani na kuitia kwenye magunia. (uk.38) Hawakujali miale mikali ya jua wala mvua za vuli au masika. Walijizatiti ilmradi wasipokonywe vijishamba vyao na bwanyenye huyo...Nao wanawake na wasichana walishinda shambani humo wakichambua pamba hiyo iliyovunwa ili kuondoa taka. (uk.39)

Enzi za ukoloni ubinafsishaji wa mashamba kwa minajili ya kupata mapato zaidi uliathiri wanajamii huku ukitupilia mbali haki za matumizi ya mashamba za kitamaduni. Shiva (1993:73-74) akiangazia mawazo ya Ester Boserup (1960) jinsi umaskini miongoni mwa wanawake ulivyoongezeka wakati wa ukoloni anaeleza kuwa, kutokana na ongezeko la upanzi wa mimea yenye mapato ya juu, mavuno ya vyakula yalipungua na wakati ambapo wanaume walihamia mijini au kufanyishwa kazi za lazima na wakoloni, wanawake mara nyingi walibakia na mapato

kidogo ya kulisha na hata kutunza familia zao. Ananukuu hitimisho la utafiti uliofanywa na Shirika la Umoja wa mataifa la wanawake ambalo liliangazia hali za kiuchumi za wanawake zilizodorora kadri mapato yalipopungua. Anaeleza kuwa,

> ...Uwezekano wa wanawake kupata mapato na ajira umedorora, mzigo wa kazi umeongezeka ilhali hali zao za kiafya za lishe na hata elimu zimepungua na kudorora.

Hali hii ya ubinafsishaji ndiyo tunayoshuhudia katika riwaya na ndiyo inayowasababishia wanawake wa kijiji cha Latimbi masaibu mengi hivyo kulazimika kumtumikia Bw. Brook ili watimize haja zao na za wanao. Ubinafsishaji huu unaathiri mazingira kwa kiasi kikubwa kwani unyunyiziaji maji mashamba ya pamba unawanyima Walatimbi uhuru wa kutumia maji safi ya mto Milu na kubakia kuyanunua kwa mifereji ya bwana huyo au hata kukosa kama asemavyo Bi. Mkubwa,

> Ni kweli anayosema Mkude, mie sina hata maji mwangu nyumbani, achilia mbali chakula.... (uk.41)

Matatizo haya vijijini ndiyo yanayomhuzunisha Nakuruto na kupelekea juhudi zake za kurejesha mfumo wa ekolojia kupitia kwa utunzaji mazingira. Juhudi za kupigania urudishaji wa mfumo wa awali katika kijiji cha Latimbi zinazaa matunda pale uhai mpya unapovuma tena kijijini. Tunasimuliwa kuwa,

> Mashamba yalilimwa na mimea anuwai kukuzwa. Watu walikuza ng'ombe, mbuzi kondoo na chochote kile kilichoweza kufugwa. Mvua zikanyesha na kijiji kikanawiri. Mto Milu ukavuma kwa wingi wa maji ambayo awali yalifujwa na

dhalimu Yule. Walatimbi walivuna vyakula wakavijaza kwenye maghala... (uk.50)

### 3.3 Pingamizi katika uhifadhi

Ili mabadiliko ya mazingira yaweze kuonekana, Nakuruto kama kiwakilishi cha wanawake wanaojali mazingira anajitolea kupigana na changamoto zote zinazomkumba ilmradi lengo lake lipate kutimia. Katika ulimwengu halisi, wanawake hupitia changamoto si haba wakati wa kuzikimu familia zao. Hata hivyo wana uhusiano na mazingira yao kwa kuyajali zaidi kuliko wanaume. Jinsi ambavyo wanawake wanatunza familia zao ndivyo hiyo wanavyotunza mazingira kwani wanazo hisia nzito ikilinganishwa na wanaume hata katika kazi za fasihi ambazo ni bunifu. Nakuruto anakumbana na pingamizi kubwa kutoka kwaumma ambao haukufahamu athari za matumizi mabaya ya maliasili na elementi nyingine za kiekolojia. Jamii hii inashikilia imani potovu kwamba mwanamke hafai kuonekana akiwa na kisomo cha juu ambacho kimetengewa wanaume. Wanajua mahali pa mwanamke ni jikoni utunzaji wa watoto na uendelezaji wa kizazi cha kibinadamu. Kwa mfano katika uk 32-33:

> Kando ya ziwa, umati wa wanawake na watoto ulikuwa ukifua nguo. Maji taka yalikuwa yakimiminiwa ziwani mfululizo. Povu la sabuni lililomwagwa mahali pale kwa miaka mingi tayari lilikuwa limeathiri mazingira ya ziwa...mmoja wa wale wanawake hakupenda jinsi Nakuruto alivyosimama pale kama sanamu. Kwahivyo, akaanza kumsibabi, "Sikujua siku hizi kuna wanawake nyapara."...Tangu lini tukawa na maafisa wanawake hapa kwetu! Hicho ni kioja bibi,"alitamka Mama Bintifundi huku akibebetua midomo, ishara ya dharau.

Kwake, wazo la kumhusisha mwanamke na kazi za ofisini lilimtia kero kwani hastahili kabisa kutwaa madaraka kama hayo. Aliamini kwamba, mwanamke daraka lake ni mekoni na kutunza watoto ili kuendeleza kizazi chabinadamu.

Baada ya kumfukuza mzungu kijijini Maweni, wanakijiji wanamlaumu Nakuruto aliyewasaidia kuwafukuza wazunguna hata kumlinganisha na mtoto mdogo anayeota ndoto. Hii ni jamii inayoendeleza ukandamizaji wa wanawake hivi kwamba hawana ruhusa ya kuongea mbele ya kaumu ya wazee, nafasi yao ni duni. Nyapara katika uchimbaji madini aliuliza,

> ...Haya yote yametokana na kuzingatia mawazo ya mtoto mdogo tu wa kike anayeota ndoto.Lakini tangu lini jamii hii ikamruhusu mtoto wa kike kuongea mbele ya kaumu ya wazee? (uk.70)

Katika harakati za kusaka nta wanavijiji wanajawa na manung'uniko mengi ndiposa Sheshije anajitolea kutumiwa kuipeleka kurunzi anakumbana na misimamo mikali ya mwanaume(Ba Ludao) anayedhani mahali pale si pa wanawake kwa kuweleza, "Mwanamke milki yake ni nyumbani sio mahali kama hapa," .

Hata kupitia kisasili kinachotolewa naye Ba Ludao ni wazi kwamba wanakijiji wanaamini kwamba mwanamke hapaswi kuaminiwa kwani ndicho chanzo cha maovu. Msimamo wa wanawake ni kuwa wanataka kuwa weledi wa kupanda ngazi. Wanawake wanataka wapewe uwezo wa kuchangia katika maendeleo ingawa wengine wao hawawezi kama mke wa Ba Kakutika. Nakuruto anakumbwa na masimango kutoka kwa wanajamii wanaomwona kama 'kisirani, kidomo ladha, kidhabidhabi binti Lusifa'. Isitoshe kunao wengine kama Mzee Saluda (uk.61) na Ba Mkude (uk.113) wanaomchukulia kama kikaragosi, kibaraka na jasusi wa wazungu.

Juhudi za kutaka kuokoa mazingira ya wanakijiji zinachukuliwa kama ndoto ya Nakuruto pale wanavijiji mbalimbali wanaonyesha kukosa uhakika na mawazo ya mhusika huyu. Leboni (82) anamweleza kuwa"Ni mustahili kushindana na upepo wa mabadiliko...Utaumia bure chaurembo" hata anapoelezewa mipango ya kuwaondoa akina Quick Buck wapya Leboni ana shauku hasa kwa maneno yake,

> Ewe msichana.Unaota nini?
>
> Naona huoti tu bali una kasoro kichwani

Ngocho haamini maneno ya Nakuruto anayetaka kuzungumza na watu waliojaa ghadhabu za malipo duni ya Bw. Mjasiri anamwona kama 'msichana tu' hasa kwa usemi wake,

> Nani? Wewe? Ha! Msichana kama wewe una lipi la kuwaambia watu wale walioiva kwa ghadhabu...

## 3.5 Hitimisho

Sura hii imejadili pakubwa jinsi ekolojia ya kifeministi ilivyo na mchango wa kumwasilisha mwanake kama mtetezi wa mazingira. Ni wazi kwamba kuna utegemezi mwingi wa mazingira upande wa wanawake kukamilisha shughuli za kimaisha ingawa si kusema kwamba wanaume hawahitaji bali ni kutilia mkazo kwamba uhusiano wa wanaume na mazingira si ule wa karibu sana hasa tukirejelea dhana kwamba majukumu ya wanawake na wanaume katika jamii ni tofauti. Ili suluhisho kwa matatizo ya kimazingira lipatikane, lazima mwendesha shughuli hii akabiliwe na changamoto kutokana na wanajamii ambao hawamwamini Nakuruto.Sura hii imetolea mifano mwafaka kutoka kwa riwaya kama idhibati.

# SURA YA NNE

## UHARIBIFU WA MAZINGIRA NA ATHARI ZAKE

### 4.1 Utangulizi

Sehemu hii imeangazia uharibifu wa mazingira na athari zake kwa wanadamu, wanyama na hata viumbe wengine. Zaidi ya hayo athari hizi zimeathiri mazingira na maumbile asilia. Athari hizi zote tumeziangazia kwa kukita kwenye matini rejelewa.

### 4.2 Uharibifu wa mazingira

Uharibifu wa mazingira hutokea kupitia matendo mbalimbali ya mwanadamu. Hata hivyo uchafuzi mkubwa unatokea kutokana na viwanda ambavyo kando na kuchafua hewa safi, taka zilizo na kemikali huelekezwa kwenye chemichemi za maji. Mwaka wa 1984 tani 40 za gesi yenye sumu kutoka kiwanda cha kemikali cha Bhopal, India zilifuja na kuwauwa watu elfu tatu na kati ya laki nne walioathirika wengi wao wameaga. Wanawake ndio walioathirika zaidi kwa kupata matatizo ya kizazi, kupoteza ujauzito na hata kuzaa watoto waliokufa. Hali hii ilishuhudiwa America eneo la Love Canal kaskazini mwa jimbo la Carolina ambapo wenyeji walioishi pale waliathirika kutokana na kemikali zilizofukiwa na kampuni ya Hooker. Kulingana na Shiva (1993:82-5) wakaazi waliathirika zaidi huku asilimia 75 ya wanawake walioishi pale wakipoteza ujauzito ilhali kati ya 15 waliokuwa wajawazito wawili pekee ndio waliojifungua watoto wasio na matatizo ya kiafya.Hizi ni baadhi ya takwimu zinazazoonyesha madhara ya uchafuzi wa mazingira.

Kando na uchafuzi wa hewa kupitia viwanda uharibifu mwingine wa mazingira unatokana na ukataji miti kiholela. Maendeleo katika mataifa yamechochea ongezeko la idadi ya watu ambao wanapenyeza kwenye misitu ili kujenga makao na majumba mbalimbali na hivyo kuendeleza

ukataji wa miti ya kiasili yenye faida kwa mwanadamu. Utafiti waSchulz (2001:201-203) katika wilaya ya Kilifi unabaini kwamba misitu ya makaya imeharibiwa kwa kujenga nyumba na hoteli za kitalii katika maeneo ya Kaya Chale ambapo ni katika kisiwa cha Chale na nusu ya kisiwa kimeshauzwa na mwenye hoteli wa. Schulz anatambua hatari nyingine katika wilaya ya Kwale ambayo ni mpango wa kujenga kiwanda cha titanium metal bila kupima athari kwa mazingira ya miti, maji, ardhi, wanyama na wanadamu.

Wanakijiji wa Maweni, Latimbi na hata Maboni wanaendeleza uharibifu wa mazingira pasi na kufahamu madhara yake. Nakuruto anatambua kwamba matendo ya wanajamii ndiyo kisababishi kikuu cha baadhi ya matatizo ya kimazingira yanayoshuhudiwa vijijini. Akiwa ukingoni mwa bwawa anashuhudia Ludao akichimba mitaro ya kupitisha maji ya ziwa shambani mwake hatua ambayo itachangia ukosefu wa maji jinsi anavyosema,

> Mitaro mingi mnayochimba mahali hapa mtakuja kukausha Ipe Ludao...

Nakuruto anashuhudia uchafuzi uliokuwa ukifanyiwa ziwa na wanakijiji ambao hawakujua hatari iliyokuwa mbele yao. Tunasimuliwa kuwa:

> Kando ya ziwa, umati wa wanawake na watoto ulikuwa ukifua nguo. Maji taka yalikuwa yakimiminiwa ziwani mfululizo. Povu la sabuni lililomwagwa mahali pale kwa miaka mingi tayari lilikuwa limeathiri mazingira ya ziwa. Miti ilikuwa imeanza kupiga manjano kwa sababu ya magadi mengi ya sabuni.

Kama mwanamke aliyethamini uhai wa elementi za kimazingira, analinganisha uhai wao unaotegemea ziwa Ipe na mtoto mchanga anayekatiziwa ziwa la mamaye. La muhimu kwake ni kutoa hadhari kwa uchafuzi wa ziwa uliokuwa ukiendelezwa na wanakijiji na kuweka wazi athari ambayo ingewakabili mbeleni akisema:

Maji taka mnamwaga humo ndani.Nyie wenyewe mnaoga humo ilhali wengine pale chini wanateka maji wakinywa.Wakulima wanazidi kuchimba mitaro mikubwa ya kupitisha maji ya ziwa mashambani mwao. Gugumaji linaloota pale ni tisho kwa uhai wenu na kizazi kijacho. Mnafahamu kuwa ziwa hili husitiriwa na mto mmoja tu. Hamna chemichemi wala vijito vinavyolisha ziwa hili.Je, likitoweka uhai wenu utasalia ?

Mbinu mbalimbali za kilimo zimechangia katika kudorora kwa elementi mbalimbali za kimazingira. Mbinu hizi zinajumuisha unyunyizaji mashamba maji kwa njia isiyofaa. Nakuruto anawaeleza Waipe kwamba mababu zao walichangia samaki kuhama hasa wale waliokuwa na bahari ya mashamba karibu na Ziwa kwani walianzisha uchimbaji mitaro na kufuja maji ya ziwa na kunyunyiza mashamba.

Uchanganuzi na suluhisho mwafaka la matatizo ya kimazingira kama vile ukataji miti kiholela, uchafuzi wa maji, kilimo na uzalishaji chakula na ueneaji wa taka yenye sumu lazima yahusiane na uelewa wa hali za wanawake na watoto. Kwa mtazamo huu tunapata picha kamili ya jinsi ambavyo wanawake wanapata matatizo uharibifu wa mazingira unapotokea kwani, miti inapokatwa watakosa kuni hivyo kulazimika kutembea zaidi kila siku wakikusanya kuni. Chemichemi za maji zitaanza kukauka kumaanisha kwamba ukame utawazonga na lazima wanawake watembee hata zaidi ili wapate maji na kuyapeleka nyumbani. Maji yanapochafuliwa, matumizi ya nyumbani kama ya udobi yatatatizika. Uzalishaji wa chakula ukiwa kwa kiwango kidogo bila shaka njaa itapiga hodi na kiwango cha maeneo yaliyo na taka yakiwa mengi afya yao na watoto inazorota.

Cheche (2009:10) katika makala ya 'Utu wa Mtu unadhihirika katika utunzaji wa Mazingira' anajadili misimamo ya wanasaikolojia ambao wanaamini kwamba matatizo mengi ya mazingira na mifumo ya kiikolojia yametokana na kukosekana kwa uhusiano wa karibu kati ya maisha ya kisasa na mazingira kutokanana watu kuhamahama. Anaeleza kwamba kukosekana kwa uhusiano huu kunaonyesha kwamba shughuli za kijamii zinashindana na malengo ya wahamiaji wanaojali zaidi ukuaji wa uchumi na kutothamini mazingira asilia. Akitolea mfano wa mgawanyo wa ardhi ni kweli kwamba wanadamu huweka umuhimu mkubwa kwenye faida watakayopata kwenye matumizi ya ardhi kuliko faida za kiikolojia.

Hata ingawa Nakuruto anadhaniwa kuwa kibarakala cha mzungu anajieleza waziwazi kwamba ni mjumbe anayetaka kupatanisha wanakijiji na ardhi yao ambayo ndiyo uhai wao. Anatambua kwamba kisababishi cha uharibifu ni tamaa ya kusaka nta yake Quick Buck ndiposa anawaeleza wazi suluhu la matatizo yao. Anaeleza kwamba :

> ...nimekuja kuwaunganisha na kitovu cha ardhi hii ili muweze kufyonza nta yake, mjirudishie afya yenu iliyozoroteshwa na wasakaji wa nta ya bw. Quick buck ...nimekuja kuwaambia kwamba uchimbaji wa visima ukome mara moja. Kima cha maji kinazidi kushuka ardhini kutokana na ukame mliosababisha nyinyi wenyewe. Miti haitamea na mvua itawapa kisogo... uchafuzi wa mazingira umetokana na mbio za walafi miongoni mwenu kutafuta harufu ya nta.(Uk.113-114)

Uharibifu huu wa mazingira una madhara kwa wanawake zaidi na hutokea kwa sababu ya vichochezi mbalimbali kama vile: ubinafsi wa matajiri unaopelekea unyakuzi wa ardhi karibu na

chemichemi,hali za ukapitalisti kuongezeka,kuwepo kwa teknolojia za kisasa na hata maendeleo ya viwanda.

### 4.2.1 Ubinafsi

Hali ya kutaka kumiliki ardhi kubwa kiasi cha kuwaacha wenyeji wengine bila ardhi ya matumizi ni jambo linalochangia uharibifu wa mazingira. Maeneo yenye chemichemi yanachukuliwa na matajiri huku kiasi kikubwa cha mashamba walio nayo kikitumiwa kukuza mimea isiyoongeza mazao ya chakula bali kilimo kinacholenga kuongeza mapato ya matajiri kutokana na mazao hayo kuuzwa nje ya nchi. Upanzi wa aina hii umechangia katika ongezeko la njaa kiasi cha kwamba kiwango cha mazao kwa minajili ya chakula kimepungua. Nakuruto anagadhabishwa na tabia ya mabwenyenye kutumikisha watu bila huruma na hata kunyakua mto uliohimili uhai wa Walatimbi hasa anapokiri kuwa,

> Zamani, Walatimbi walimilki maji ya mto huu ambao walizawadiwa na maumbile. Uhai wao ulitegemea mto huu. Lakini sasa uhai wa watu hawa unadhibitiwa na bwanyenye anayewatumikisha bila huruma...uhai wao unatishwa na nguvu za mamlaka kutoka nje ya kijiji.

Tunasimuliwa jinsi wanakijiji walivyohangaishwa na Bw. Brook, hali inayompa Nakuruto wazo la kumwondoa

> Aliutazama mto ule jinsi ulivyobinafsishwa na mtu mmoja huku kijiji kimoja kikisota bila maji. Bw. Brook aliyamiliki maji yale akawanyima wanakijiji kuyateke kwa matumizi yao ya nyumbani.... Bw. Brook aliwapokonya wanakijiji ardhi ili kuendeleza kilimo cha pamba. Wanakijiji hawakuwa na jingine ila

kulihudumia shamba lake ili kukatiwa vijishamba ambamo walikuza mazao yao duni....Pamba iliyochambuliwa na kusafishwa ilisafirishwa kwa malori nje ya kijiji na madahuli yote yalimwendea Bw.Brook, mwenye shamba. (uk.38)

Katika kijiji cha Maboni baadhi ya wenyeji walimiliki mashamba kinyume cha serikali na kujenga katika ardhi ya umma. Jamaa za Leboni ni miongoni mwa wabinafsi waliochukua ardhi iliyoachwa na 'mahaini' kama anavyotaja.

...Wengine tulijitwika ubinafsi wa madhalimu wale, tukafwata nyayo zao sawsawa. Tulianza kuparamia ardhi kwa pupa ya kihayawani. Wengine tukachukua ardhi zilizotengewa makaburi na wengine tukanyakua hata viwanja vya shule...

Ubinafsi huu unaleta madhara zaidi kwa wanawake ambao wanadhoofika wanapofanya kazi juani huku watoto wakipokezana vilio. Kwa kuwa shamba ni sehemu muhimu kwa maisha ya mwanamke, lazima pia ashughulikie kijishamba chake kidogo baada ya kazi.

Matokeo ya ubinafsi huu ni tatizo la uskwota na hata watoto wa shule ya Majaaliwa kusomea chini ya mbuyu huku mahali walipopaita shule pakiwa pamezungushiwa seng'eng'e. Matajiri wanaosaka harufu ya nta wamevua utu wao na kufurusha watu katika mastakimu yao. Tunasimuliwa kuwa,

Kweli kabisa. I swear ardhi hii yote itakuwa yetu.Ndoto yetu imetimia sasa ...hata nta tutaimiliki. Kiwanda cha ngozi nakiona kwa karibu sana.... (uk.87)...Watoto wale ni wa shule ya msingi ya Majaaliwa. Hivi majuzi walitimuliwa kutoka katika shule yao na tajiri mmoja aliyedai shule hiyo ilijengwa katika ploti yake (uk.88).... Walipita katika mtaa mwingine ambapo waliona watoto wengine

wakisomea ndani ya mahema. .... Walitimuliwa kutoka katika shule yao na majengo kubomolewa kwa kutumia matingatinga. ....Amini usiamini, takriban majengo haya yote yanavuma umati wa wakimbizi kutoka vijiji jirani...Baadhi yao walichomewa nyumba, wakafurushwa kutoka mastakimu yao na mabedui hao wasiothaminiutu wa binadamu... (uk.90)

Nakuruto anapokumbuka siku za utotoni mwake anakumbuka kijiji cha Maweni kilichokuwa na vibarua wengi ambao wamesalia katika lindi la umaskini kwa sababu ya sera mbaya zinazoendeleza ubinafsi. Anaeleza,

> Mabarakala wale waliishi kunyonya jasho la Wamaweni huku wakistarehe kwa mvinyo na chakula ...nahisi mambo yanazidi kuzorota...Joto hili linalochoma ni ishara ya uharibifu wa maliasili. Ardhi iliyomilikiwa na wachache sasa imekuwa yabisi kwa kufujwa na wanyonyaji wale. (uk.53)

### 4.2.2 Teknolojia na viwanda

Mataifa mengi yaliyoendelea yamelikumbatia swala la teknolojia ya kisasa huku yale yasiokaribisha teknolojia yakionekana kubakia nyuma. Teknolojia imekuwa na madhara yake kwenye ekolojia kando na kufaidi mwanadamu kupitia uvumbuzi unaotokea kila uchao.Teknolojia imeingizwa kwenye kilimo ili wanadamu wapate mazao maradufu lakini wanaufeministi wa kiekolojia wana maoni tofauti. Ubunifu wa kiteknolojia katika kilimo, nishati, matibabu na hata kwenye viwanda umetoa mwendelezo wa ukuaji wa maisha ya mwanadamu. Teknolojia mpya za kilimo zinazohusiana na matumizi ya maji, mbolea na ufugaji imebadilisha sekta ya kilimo, na kuleta ongezeko la mazao. Hata hivyo maswali yameibuliwa

kuhusu uwezekano wa kukimu mahitaji ya kesho huku asilimia 11 ya ardhi kote duniani ikiwa inatumika kwa ajili ya kilimo na hata sehemu zingine kuwa na nafasi duni ya kupanua kilimo kwa sababu ya ardhi isiyotosha au ukosefu wa maji kulingana UNDP (2005). Teknolojia inayo uwezo wa kuongeza kiwango cha mazao na wakati huo huo kuchangia katika uharibifu wa mazingira hasa kupitia kemikali zinazotumika kwenye kilimo kupenyeza ndani ya mito, maziwa na hata bahari.

Katika kilimo wanawake ambao ni wakulima wanajua kuwa mbegu ndio mwendelezo wa kizazi lakini kampuni mbalimbali zimeibuka na uwezo wa kutengeneza mbegu ambazo haziwezi kamwe kutumika tena kuendeleza vizazi. Katika harakati za kusaka nta wanavijiji wanaingilia mitindo ya ughaibuni na kutupilia mbali uasili.Hata mimea inayokuzwa inatoka ughaibuni. Tunasimuliwa kuwa,

> Wanavijiji wengine waliacha kukuza vyakula vyao vya kiasili... mashamba yakakuzwa mimea kutoka ughaibuni...Hata samadi pia zilitoka huko huko kwani zile za kiasili ziliambiwa zinafukuza harufu y anta.... Wanavijiji waliacha kukuza mimea iliyohimili mazingira ya asili yao na kukuza ile isiyokubali mazingira yao... (uk.101)

Hali ya wanakijiji kusaka nta kwa kutupilia mbali uasili wao ndiyo inayompa machungu mhusika Nakuruto ambaye anapigania uasili na uhifadhi wa mazingira kwani anahisi kwamba harakati za kusaka mali zote huishia katika uharibifu wa sayari ambayo ndiyo mhimili wa uhai wa wanavijiji. Harakati za kusaka nta zilipelekea uharibifu wa mali asili kutokana na uchimbaji wa madini na uvunaji wa mchanga. Nakuruto anaona kuzoroteka kwa afya ya wanavijiji kutokana na mahangaiko ya kusaka dafina ya Bw. Quick Buck. Kuwepo kwa kiwanda cha

pamba kunawafanya baadhi ya wanavijiji kutupilia mbali upanzi wa vyakula almuradi waweze nao kunusa nta. Tunasimuliwa kuwa,

> ....Mashamba ya vijijini yaliacha kulimwa, watu wakakimbilia mashamba makubwa makubwa yenye kuzalisha mazao ya kusafirishwa nje ya vijiji. Konde za watu zikamea magugu kwa kukosa huduma. Hata wale waliokuwa wakilima ili kukidhi mahitajia yao, walitenga ardhi kubwa ya vikataa vyao kukuza mazao yaliyoweza kutega harufu ya nta.... (uk.140).

Katika dondoo hili ni wazi kwamba hali ya kutaka kujiendeleza kiviwanda na kiteknolojia ilikuwa na madhara hasa kwa wale wasiokuwa na elimu ya kutosha hivi kwamba wanatupilia mbali shughuli za kilimo cha vyakula na kuishia kufuata taratibu za wasakaji nta ambao ni mabwenyenye wasio na taabu ya kupata chakula. Ndiposa Maridhi na vijana wengine wanauliza,

> ...Kwa nini wasikae pamoja wakashirikiana na kuunda mikakati iliyokita kwenye ujamaa wao wa kiasili? Kwa nini wasitumie utaalamu huo wa kusakura wavuti wa Quick Buck ili ufaidi wanavijiji badala ya watu wachache? Hatuna budi kujielewa sisi wenyewe kabla ya kupapia mageni tunayodhani yatatunufaisha sisi sote (uk.143).

Ulimwengu wa sasa unakumbwa na njia panda ambayo inatokana na matumizi ya teknolojia ya kisasa ili kuongeza kiwango cha mazao kwa kutumia mbegu zilizofanyiwa uchunguzi wa hali ya juu na hali ya kuhifadhi ubora wa rutuba kwa matumizi ya mbegu za kiasili. Lahar (1991:32) anaangazia swala la mapinduzi ya kijani kama mbinu za kilimo zilizoingia katika teknolojia ya kisasa na ambayo ipo kwenye mataifa yaliyoendelea na kuingizwa kwenye mataifa yanayoendelea hasa kupitia haja ya kutaka kukuza mimea yenye faida ya juu ili kulipia madeni

waliyonayo. Mbinu za mapinduzi ya kijani zinajumuisha kukuza mimea kwa matumizi ya mbegu spesheli zinazostahimili wadudu, kemikali zinazozuia wadudu na unyunyizaji maji mashamba. Mapinduzi ya kijani yamechukua mahala pa mbinu za kitamaduni ambazo zilihimili rutuba ya mchanga na kuhusisha ukuzaji wa mimea na vyakula tofauti tofauti kila msimu hali iliyoongeza rutuba na kuangamiza wadudu. Mbinu za kiasili na kitamaduni zilijumuisha ufugaji wa wanyama na upanzi wa miti kama njia ya kuongeza rutuba shughuli ambazo zimepotea katika mapinduzi ya kijani yanayojali zaidi kilimo cha hali ya juu kinacholeta mapato mengi baada ya muda mfupi.

### 4.2.3 Ukoloni

Mataifa yaliyokolonishwa yaliibuka na matatizo ya kimazingira na umaskini kutokana na maliasili kuchokolewa na kupelekwa kwenye mataifa koloni.Ukoloni na ukapitalisti ulibadilisha ardhi na mchanga kutoka kwa chemichemi ya uhai uliyohimili watu hadi kwenye mali ya kibinafsi inayoweza kununuliwa na kuuzwa na kutwaliwa na watu binafsi kwa minajili ya maendeleo (Shiva,1993:105).

Baadhi ya wanawake waliohusishwa katika vuguvugu la Green Belt Movement hapa Kenya lililoendeleza upanzi wa miti na uhifadhi wa mazingira, wanashiriki wazo moja kwamba zamani sana kabla ya kuja kwa wakoloni, sehemu zote zilikuwa na miti ya kiasili na kutokana na miti hii, maji na kuni zilikuwa nyingi. Maisha hayakuwana shida kama ilivyo sasa. Nakuruto anadai kwamba ikiwa wanakijiji wa Ipe wanataka kuishi maisha mema, lazima wamwondoe Bw Brook, Bw. Quick Buck na wanyonyaji wengine ambao ni ishara ya mkoloni, mkoloni mamboleo na athari zake. Nakuruto anawakemea kwa kusema kwamba:

> Nani kati yenu asiyejua kwamba zamani Latimbi ilikuwa na shibe ya kusifiwa? Ni kwa sababu mmefarakana na ardhi yenu.Hamkuitunza ipasavyo ...Leo hii mnataka kuifuja zaidi kwa upanzi wa maua yasiyowafaidi. Niulizeni kwa nini kijiji hiki hakina idadi kubwa ya wananchi kama zamani au kwa nini vijana walioelimishwa kutokana na mavuno ya ardhi hii wamehamia vijiji vingine? Ni kwa sababu wamo mbioni kuitafuta harufu ya nta kwa udi na uvumba. Wale waliopata hawataki kurudi tena.Sasa wamo mbioni kuitafuta nta iliko. Miti mikuu iliyokuwa hapa imekatwa na mbao kuuziwa matajiri walionusa nta. Ardhi yenu mkaigeuza jangwa yabisi lisiloweza kuzalisha chochote.

Dondoo hili linaonyesha jinsi ambavyo msanii kupitia kwa mhusika mkuu anakerwa na mfumo wa kiuchumi unaokandamiza mazingira. Ni dhahiri kwamba licha ya waafrika kujinyakulia uhuru miaka ya 1960, hawakujali waafrika wenzao bali waliendeleza hulka za kiuchumi na ujasiriamali wa kizungu. Tabia hizi baadaye zimeathiri mazingira kwani viongozi wa Kiafrika hawakuweka sera za utunzaji mazingira bali uharibifu wa ekolojia, ulimbikizaji mali, unyanyasaji wa kitabaka na kijinsia, na siasa mbaya ndio dhana zilizotawala waafrika hawa. Waliuza misitu ekari kwa ekari kwa lengo la kujenga majumba ya kifahari, kukuza mimea ya kuuzwa nje ya nchi na kujipatia uwezo mkubwa wa kiuchumi ili walingane na viongozi wao katika nchi zilizoendelea. Nchini Kenya, misitu kama vile Mau ina tisho la kuangamia kutokana na ukataji wa miti na watu walio na ushawishi mkubwa serikalini na ambao walimiliki sehemu hizi.

Kipindi cha ukoloni, kazi nyingi zilizokuwepo zilitendwa na wanaume ambao walitumikishwa zaidi hasa katika mashamba ya manyapara wa kizungu. Muthuki (2006:19-20) katika tasnifu yake, akinukuu mawazo ya Mies (1998), Oyewumi (1997) na Shaw (1995) anadokeza kuwa,

utawala wa kikoloni uliweka wazi tofauti za kimajukumu kati ya wanawake na wanaume huku wanaume wakipendelewa zaidi katika nyanja za elimu na ajira. Katika majilio ya uchumi wa kikapitalisti wanawake walibaki nyuma na kulazimika kutegemea wanaume. Hivyo basi utawala wa kikoloni ulikuwa na sifa ya kuwaacha nyuma wanawake katika maswala muhimu. Akimnukuu Kanogo ( 1992), Muthuki anaeleza kuwa, wakati wa utawala wa kikoloni nchini Kenya, kulikuweko na mabadiliko ya matumizi ya mashamba na mifumo ya kilimo na ugawaji mkubwa wa mashamba uliofaidi wazungu na kuleta athari kubwa kwa jamii za vijijini. Ni wakati wa enzi hii ndipo wakoloni walipojinyakulia mashamba na wakati huohuo wanavijiji wengi kupoteza vipande vyao vya ardhi, hali iliyowaletea wanawake matatizo mengi kwani hawakuruhusiwa kukata kuni kutokana na ubinafsishaji wa mashamba.

Baadhi ya wanakijiji wanakiri kwamba walimpa mzungu ardhi hata akajenga kasri karibu na mto. Kwa kufanya hivyo, matumizi ya maji kutoka kwa mto huo yalikatizwa na hata kuchangia kushuka kwa maji. Uchungu walio nao wanawake ni kwamba mkoloni huyo aliwapa dhuluma tupu na kuwaongezea ukata ilhali yeye mwenyewe kujinufaisha. Mwanamke huyo anaeleza kuwa,

> Hakuna jema aliloleta ila dhuluma na ukata mtupu.Tazama jinsi tulivyofukarishwa na bahili yule huku tukilijaza tumbo lake kwa mazao ya jasho letu.

Maskwota wamejaa kwa sababu ardhi iliyokuwepo imenyakuliwa na mabwanyenye wenye uchu na ulwa wa kujasiriamali na kukiritimba sekta zote za kijamii kwa faida yao, familia zao na marafiki zao. Mtunzi wa Nakuruto anawaita vitimbakwira. Wananchi maskini wanahama sehemu zao na kwenda sehemu ambazo rasilimali ipo kwa ajili ya kuchumia kifuutomo.

Nakuruto anashuhudia hali mbaya wanamojipata wanavijiji kutokana na tamaa ya mabwanyenye wasio na utu. Katika sura ya saba, tunatambua kwamba anapigania usawa wa kijinsia na haki za binadamu dhidi ya watawala wa kikoloni mamboleo. Watawala hawa wamewateka nyara mafalahi huku wakiwatumikisha kwa manufaa yao kiuchumi. Misaada ambayo wanapata kujiendeleza kiuchumi kama jamii inaporwa, inafisidiwa na watu binafsi wenye uchu wa kupata harufu ya nta ya Bw. Quick Buck (uk. 126-129). Kuhusu haki za wanawake, Nakuruto anashadidia wazo la Nashelengai anayesema kuwa, "wanawake siku hizitunataka kuwa weledi wa kupanda ngazi…" (uk.132-133), Nakuruto anasema kwamba;

> …bora tu ajiheshimu na asikubali kuvaa sifa za kutukuza nafsi yakiume na kuikashifu ile ya kike (uk.133).

Mkoloni mwingine aliyeleta madhara kwa wenyeji ni Wellingtone ambaye alikuja na vibarua wake wa kazi. Mawazo yake ya kuwepo kwa mgodi yanachangia pakubwa katika kudorora kwa mazingira na hali za Walatimbi. Anaendeleza uhamiaji wa wanakijiji katika katika ardhi nyingine na kuendeleza uchimbaji wa madini. Kwa kukosa lishe inawabidi waingilie shughuli zilizo haribifu ili kujikimu kimaisha. Mzee Saluda anakiri kwamba:

> ...Wengi tulilazimika kuchoma mkaa na kwenda kuuza katika vijiji jirani ili kujinusurisha...Hadi sasa mvua hazinyeshi. Zitoke wapi na mitiimekatwa yote...Baada ya kumaliza miti waligeukia mchanga. Waliteka mchanga wakaukusanya mafungu na kuwauzia wajenzi wa makasri yaleee... (uk.57)

Licha ya Wazungu hawa kuwa wakoloni, wanaendeleza mfumo wa kikapitalisti ambao unawafaidi peke yao. Wanafaidika kutokana na madini kwa kuisafirisha ughaibuni na kujirundikia hela nyingi na kuwatelekeza wale waliowaachia ardhi. Isitoshe hata baada ya

Wanguzu hawa kuwapa watoto mafunzo hawawezi kuwaajiri bali wanawaajiri watu wa ughaibuni wenyeji wakibakia kufanya kazi zisizo na kipato kikubwa.

Wazungu wanapoondoka wanaacha viwanda na mashamba ambayo yanachukuliwa na akina 'Quick Buck' wapya. Hizi ni nafsi za ukoloni mamboleo ambao wanabaki na mali ya mkoloni na huendelea kumnyanyasa mwanakijiji. Kama anavyoelezea Nakuruto, waasisi hawa wa ukoloni mamboleo wanawahangaisha wanakijiji hata kuliko wakoloni wa mwanzo. Wanachangia katika matatizo ya ukosefu wa chakula wanapoweka minara mirefu ya mawe kwenye mashamba yenye rutuba. Akimweleza Leboni, Nakuruto anasema,

> .... Mashamba yale makubwa yako wapi sasa? Karibu yote yako mikononi mwa akina Quick Buck wapya.... Tazama jinsi walivyogeuza ardhi yenye rutuba kuwa minara mirefu ya mawe.... Tazama jinsi wanavyowahangaisha wanakijiji hapa toka mtaa mmoja hadi mwingine... (uk.82)

Matatizo yaliyoletwa na wazungu hawa yanawaathiri pakubwa wenyeji wa vijiji mbalimbali kutokana na madhara yanayotokea baadaye. Nakuruto kama mwanamke aliyejitolea kubadili mazingira anatoa mpango wa kubadili maafa kwa kutaka wanavijiji kujiingiza katika matendo ya kuwarudishia uhai. Mifumo ya ukapitalisti na ukoloni imesambaratisha mifumo ya kiekolojia kwa kuathiri mazingira. Unyakuzi wa ardhi lazima ukabiliwe vilivyo jinsi anavyofanya Nakuruto na hata kuondoa wanyonyaji ili faida ya mazao iwarudie wenyeji

### 4.3 Athari za uharibifu wa mazingira

Ulimwengu wa sasa unashuhudia uharibifu wa mazingira ambao umezua athari si haba katika sekta mbalimbali za jamii yetu. Nchini Kenya, misitu kama vile ya Mau, Kakamega, Arabuko na mingineyo inashuhudiwa uharibifu wa mazingira kila uchao.Misitu hii inaangamizwa kutokana na idadi kubwa ya watu inayoongezeka na kuweka makazi yao katika eneo lililotengewa misitu. Katika makazi ya mabanda, kunashuhudiwa rundiko la taka za kila aina na kububujika kwa maji machafu yaliyo hatari kwa afya ya watu wazima na hata hatari zaidi kwa watoto wachanga wenye umri wa chini ya miaka mitano. Isitoshe, taka kutoka viwanda mbalimbali zinaelekezwa kwenye chemichemi za maji na hata kuhatarisha zaidi maisha ya viumbe wanaotegemea maji hayo. Uharibifu huu umepelekea kuwepo kwa matatizo mbalimbali ya kiafya kwa binadamu. Benki ya Dunia mwaka wa 1992 ilibainisha athari za matatizo ya kimazingira kwa afya na uzalishaji. Ripoti hii ilieleza kuwa, uchafuzi wa maji na ukosefu wa maji,uchafuzi wa hewa,mrundiko wa taka zenye sumu,mmomonyoko wa udongo na ukataji miti ni mambo yanayopelekea vifo vya watu na wanyama na hata vifo vya bioanuwai. Ripoti hii inakadiria kwamba kuna vifo zaidi ya milioni mbili na mabilioni ya watu wanaougua kila mwaka kutokana na uchafuzi wa maji. Kuhusu uchafuzi wa hewa, ripoti hii inaeleza kuwa Uchafuzi wa hewa mijini ndicho chanzo cha vifo zaidi ya laki tatu kila mwaka na hata kusababisha magonjwa sugu kwa watu wengi wao wakiwa wanawake na watoto katika maeneo maskini ya vijijini.

Ukataji wa miti umepelekea mmomonyoko wa udongo, mafuriko na vifo vya bioanuwai. Uharibifu wa mazingira hurudisha nyuma maendeleo na hata kutishia maendeleo ya kesho kwani maliasili kama vile: maji mimea na hata wanyama huzunguka maisha ya mwanadamu. Kuzorota kwa mazingira hutishia maisha huku anayeathirika zaidi akiwa binadamu ambaye uhai wake unategemea mazingira pakubwa. Binadamu anahitaji lishe iliyo bora, maji safi ya kunywa na

hata matumizi mengine ya kinyumbani, anapatwa na magonjwa sugu ambayo tiba yake ni ghali, mifugo wanaathirika na mfumo mzima wa ekolojia unaathirika. Katika riwaya teule, utafiti wetu ulipata nukuu, dondoo na sehemu zilizomulika uharibifu wa mazingira. Mhusika Nakuruto anaweka bayana uharibifu huu na madhara yake hivyo basi tuliweza kujadili athari hizi kwa mwanadamu, kwa wanyama na viumbe wengine, na kwa mazingira yenyewe.

### 4.3.1 Athari kwa mwanadamu

Binadamu ndiye mwasisi wa uharibifu wa mazingira na ndiye pia mwathiriwa mkuu wa uharibifu huu. Athari ya kwanza inayomfika ni ya matatizo ya kiafya yanayoletwa na magonjwa mbalimbali kama vile saratani na matatizo ya kupumua ambayo mwisho wake ni vifo. Matatizo haya yanaibuka kutokana na kupumua hewa yenye sumu za viwandani. Mzee Saluda anamweleza Nakuruto athari iliyoletwa na kiwanda cha kusafisha madini,

> .... Isitoshe, mjukuu wangu, kiwanda hicho kimekuwa tisho kwa uhai wa wanakijiji. Hewa ya sumu itokayo kiwandani imesababisha vifo vya watu, wakiwemo watoto.Wanaoathirika huanza kukohoa kisha hupata shida ya kupumua. Baadaye huzirai na kufariki. Juzi tumemzika mtoto wa mzee Menga ambaye alifariki kwa sababu hii.

Mzee Saluda anatupa taswira kamili ya athari ya vifo na magonjwa kwa wanakijiji na hata watoto. Hali inayosimuliwa na Mzee Saluda sio tofauti na ile inayoshuhudiwa hapa nchini kwani watu wengi wameathiriwa na moshi wenye sumu unaotoka kwenye viwanda vyetu. Ripoti ya Benki ya dunia maka wa 1992 inakadiria kuwa uchafuzi wa hewa kutokana na moshi wa viwanda unawaua watu laki tatu kila mwaka huku wengi wakiwa wanawake na watoto. Ingawa

ripoti hii haitoi takwimu za wanaume wanaoathirika muhimu ni kuelewa kuwa athari hizi zinamwathiri kila mwanadamu. Kulingana na Kilabuko na Madete (2010:10) uchafuzi wa hewa una madhara yenye sura nyingi. Inaelezwa kuwa uchafuzi wa hewa huathiri afya ya binadamu, mifumo ya kiikolojia, kilimo na vitu vinavyotengenezwa na binadamu na hivyo kuathiri uchumi na ukuaji wake. Katika utafiti wao, wahanga wakuu wa uchafuzi wa hewa ni watoto kwa kuwa miili ya watoto inachukua uchafuzi kwa haraka kuliko watu wazima. Aidha, watu wenye umri mkubwa na wagonjwa wako kwenye kundi la watu walioko kwenye hatari kutokana na upungufu wa kinga mwilini.

Kando na vifo vya watu katika kijiji cha Maweni kusababishwa na magonjwa yanayotokana na uwepo wa kiwanda cha madini, Mzee Saluda anaongezea sababu ya vifo kuwa machimbo ya madini,

> Wengine wameangukiwa na majabali humo wakazikwa wakiwa hai. Wengine wamezirai humokutokana na ukosefu wa hewa ya kutosha na wengine mvua zikanyesha, mashimo yakajaa maji na kuwazamisha kabisa.

Ukosefu wa ajira miongoni mwa Wamaweni ndicho chanzo cha maafa haya kwani matajiri wamechukua nafasi katika kiwanda na kuwaajiri watu wao huku vijana wakibaki na kazi za aibuaibu. Hata ingawa machimbo haya yana maafa wanakijiji wanaendelea kuathirika pasi na kutambua wanayo suluhu hadi Nakuruto anapowafumbua macho kuona uharibifu wa udongo ulio mhimili wa uzao wao ambao umeifanya ardhi kuwa kame yabisi kama tumbo la tasa lisiloweza kuzaa chochote.

Athari kubwa zaidi inayomkumba mwanadamu ni umaskini na ukosefu wa chakula unaoishia kwa kuwepo kwa njaa. Pana uhusiano mkubwa kati ya uharibifu wa mazingira na umaskini.

Uzorotaji wa mazingira husababisha umaskini kwani ni uharibifu wa maliasili ambayo inategemewa zaidi na watu walio na mapato ya chini na kwamba athari za uharibifu wa mazingira kwa afya ya watu hupunguza uwezo wao wa kukuza vyakula. Pia, umaskini ni sababu ya uharibifu wa mazingira kwa sababu jamii maskini hujipata katika sehemu zisizo na mchanga wenye rutuba na huishia kuharibu maliasili kidogo iliyopo kaika harakati zao za kujikimu kimaisha hasa wengi wao wanapotolewa kwa lazima kwa mashamba yao yenye rutuba. Kulingana na Maembe na Mudiguza (2010:5) uharibifu wa mazingira husababisha umaskini kwani hupunguza upatikanaji wa maji safi, rutuba katika udongo, bidhaa na huduma nyingine muhimu kwa afya na maisha ya binadamu.Umaskini nao husababisha uharibifu wa mazingira kwani hudhoofisha juhudi na uwezo wa binadamu kusimamia na kutumia raslimali kwa njia endelevu.

Wito wa kutunza mazingira ili kuepuka umaskini unatiliwa mkazo katika hotuba ya Makamu wa Rais wa Tanzania Dkt. Ali Mohamed Shein alipofungua maadhimisho ya siku ya Mazingira ya Afrika yaliyofanyika mjini Arusha mwanzoni mwa mwezi Machi mwaka wa 2010 kulingana na Ameir (2010:3-4). Mbali na kutoa wito huo alisisitiza umuhimu wa matumizi ya maarifa hayo katika kulinda na kuhifadhi bionuai ambayo aliifananisha na 'bima yamaisha'kwa uhai wa binadamu. Aliwaeleza washiriki wapatao 300 kutoka barani Afrika na kwingineko duniani kuwa watu wengi barani Afrika ikiwemo Tanzania wanategemea rasilimali za mazingira katika shughuli zao za kujipatia kipato, kukidhi mahitaji yao yamsingi, vifaa vya ujenzi,nishati na matibabu.Alibainisha kuwa "utajiri wa rasilimali hizo za mazingira yaani misitu,maji baridi, bahari na rasilimali nyingine ndio mhimili wa uhai wa binadamu" na kuongeza kuwa kwa kuzingatia ukweli kuwa asilimia 45 ya miti nchini Tanzania inatumika kwa tiba asilia ni uthibitisho zaidi kuwa ustawi wa binadamu unategemea mazao na huduma toka bionuai hiyo.

Umaskini unashuhudiwa katika kazi teule kama athari inayotokana na uharibifu wa mazingira.Nakuruto katika hali ya uzee anayakumbuka yaliyojiri kijijini walipoishi na watu kama mzee Magoji anaeleza kuwa chakula hakikuwa tatizo kama ilivyo sasa. Aneleza,

> ... Hakukuwa na ukame kama siku hizi. Vyakula viligombania nafasi katika maghala na mvua zilinyesha kila wakati. Leo mvua zitoke wapi ikiwa wakongwe wanalishwa viunga wana wa ng'ombe? (uk.15)

Katika kumbukumbu zake Nakuruto wakati wa utotoni, kijiji cha Maweni ndipo mahali walipotumwa kutafuta kuni na ndipo umaskini ulikuwa umekithiri kutokana na ubinafsi wa watawala. Hali hii ilitokana na wachache kumiliki mali wengine wakibaki kama watumwa. Mabarakala anaowataja miongoni mwao ni wakoloni waliofaidi jasho la Wamaweni na kuhasiri mazingira hivi kwamba joto linazidi kuongezeka. Ni kijiji ambacho majumba yake hayakuhitaji kuelezea hali ya wenyeji kwani yalithibitisha kwamba mtaa ule ulikuwa wa mafalahi huku wakitegemea kisima kimoja kwa matumizi ya kinyumbani. Mhusika Nakuruto anashuhudia taswira ya unyonge unaomfanya kujiuliza,"ile ni kambi ya wafanyikazi au ni mtaa wa mafalahi wa kijiji hiki?" Tunasimuliwa kuwa,

> Nakuruto aliweza kuviona vijumba vya udongo vilivyoezekwa kwa makuti. Vingine vilikuwa vimebomoka kiasi cha kuweza kuwaona walio ndani. Vingine havikuwa na madirisha bali vitundu tu mfano wa viota vya ndege.Vijumba hivyo vilingangania nafasi ndogo vilivyotengewa. Kutokana na mnganganio huo, viliweza kuonyeshana migongo ilhali vingine vikitazamana...Katikati ya vijumba hivyo aliweza kuona kulikuwa na kisima ambapo aliweza kuona wanawake na

> watoto wakiteka maji. Wengine walikuwa wakifua nguo kando ya kisima... (Uk.54-55)

Hali ya kutamausha ipo kijijini humu kutokana na mababiliko makubwa hasa Nakuruto anapokikumbuka kilivyokuwa zamani sasa ni mahame hasa anapotamka, "Kijiji cha Maweni kimebadilika jinsi hii?" ilibidi wenyeji wahamie Maboni. Hiki ni kijiji kilichojivunia furaha ya kilimo kupitia maelezo ya mwandishi,

> Kila sehemu ya ardhi ililimwa, watu wakajaza mazao katika maghala na mabohari. Watu kutoka katika vijiji jirani walimiminika huko kununua mazao ya kila aina, na kijiji kiliweza kulisha idadi kubwa ya watu. Masoko makubwa yalijengwa, wanakijiji wakaanza kuchuuza mazao yao na kujipatia faida kubwa. (uk.117)

Taswira ya uharibifu wa mazingira Maweni ni ishara tosha kuwa tatizo la kimazingira linaloletwa na mwanadamu linamsababishia mwanadamu mwingine makali yasiyoelezeka na huwa tatizo kubwa kwa wanawake ambao wanalazimika kukimu familia zao kwa chakula na maji safi. Nakuruto anashuhudia makazi ambayo ni vijumba vidogovidogo visivyo na mpangilio, watoto nao kuwa nusu uchi. Isitoshe, kina mama wanayo madebe ya maji vichwani wengine wakijitwika matita ya kuni na wana migongoni. Tunashuhudia hali ya ukosefu wa chakula katika kijiji cha Latimbi ambacho zamani kilinawirishwa na mto Milu ambao sasa kima cha maji kimeshuka kwa sababu ya ukataji miti ishara ikiwa visiki vyeusi ndivyo vilivyokumbana na mboni za macho yake mhusika. Miti ya kiasili kutoka kwenye misitu imekatwa matokeo yakawa,

> ...kijiji kimegeuka kuwa tambarare lililotapakaa visiki na vijumba vya mafukara.Hata yale mashamba makubwa yaliyozalisha vyakula vya kiasili kama mawele mtama, maboga na mayungwa sasa hayako jamani. (uk.108)

Mhusika Nakuruto anachukizwa na ulitima uliokita kijijini hivi kwamba makazi nadhifu ni kitu adimu kwani vijumba viliezekwa kwa makuti na nyasi nazo nyuso zilizosinyaa kwa kukosa lishe bora zikisitiriwa na wanakijiji.Tunaelezewa kuwa,

> Wanakijiji walisalia kufanya kazi za kijungu jiko tu. Kwao maisha yalikuwa kifuu kitupu, hakuna matumaini ya kesho yenye heri.Alijionea uharibifu wa mazingira uliowatumbukiza Walatimbi kwenye lindi la uchochole.

Tatizo hili la ukosefu wa chakula bora cha kiasili linaakisiwa pia miongoni mwa wanawake wa Green Belt Movement ambao walidai kwamba wanawake wengi, hasa vijijini walianza kuteseka kwa sababu hawakuwa na kuni na maji ya kutosha kupika. Aidha vyakula vya kiasili vilivyohitaji nishati nyingi kupikika vilianza kupotea kwani kina mama hawa walinunua vyakula vilivyosanifishwa zaidi na vilivyogharimu nishati kidogo kuiva. Vyakula hivi vilikosa lishe kama vile protini na vitamin, watoto walianza kudhoofika afya kutokana na vyakula hivi. Tatizo lilitambulika kuwa ni uharibifu wa mazingira na suluhu likawa ni kupanda miti mingi ili kurejesha asilimia ya miti ya kiasili iliyokuwa imepotea.

Katika kazi teule, harakati za kusaka nta zimesababisha urumo wa hali ya juu hadi wanakijiji kubakia kufanya kazi za kuchimba visima huku vicheko vya wanawake vikifasiriwa kama vya watu waliooficha masumbufu makubwa ya moyoni (uk.109). Ukosefu wa lishe umechangiwa na haja ya matajiri walionyakua ardhi katika vijiji mbalimbali kutaka kujitajirisha haraka kutokana na upanzi wa mimea isiyo ya chakula. Kilimo cha pamba hakina manufaa kwa wanavijiji kwani

wamechoshwa nacho hivi kwamba kimechangia wao kukosa cha kutia tumboni jinsi mwanamume aliyesimamishwa na Nakuruto anavyotaja:

> Tangu asubuhi sijatia chochote tumboni.Wanangu wametoka mabebe, hawana lishe, hata mbavu unaweza kuhesabu. Mke wangu...aah wacha tu. Kabakia kifyefye, gofu la mtu.Ukimpuliza anaanguka.Kabakia ng'onda utadhani namnyima chakula.Chakula kitoke wapi bibie? (uk.40) Mkude anaongezea "mie mke wangu ametorooka.Kahamia kwao na kachukua mbuzi, mbwa, hata paka.Ningewalisha nini mie?

Matajiri wanaosimamia viwanda wanahakikisha kuwa kiwango cha mazao kwenye maghala hakiongezeki kwa kuingilia kilimo kisicho cha vyakula. Kando na kuwepo na kiwanda cha kusafisha madini, matajiri hawa wanataka kuanzisha kiwanda kingine; kiwanda cha ngozi. Bw.Mabavu Bin Mahela na wenzake wanawatimua watu kwenye ardhi yao madhumuni yao yakiwa ni kusaka nta na kuimiliki.

Nakuruto anatambua kwamba hata ingawa Bw. Brook alitimuliwa bado maruweruwe yake yanaonekana kupitia kwa Bw. Mjasiri anayewanyanyasa wanakijiji kwa malipo duni nia yake ikiwa kuanzisha kilimo cha maua ili ayasafirishe nje ya kijiji. Mipango ya kutotilia maanani kilimo cha mazao ya chakula kinasababisha njaa miongoni mwa wanavijiji ambao ardhi zao zilinyakuliwa na baadaye. Nakuruto anawasikitikia vijana wanaobeba majembe kuchimba visima ili kupata vibaba vya unga. Hata baada ya kuinyonya ardhi anashangazwa na juhudi za baadhi ya wanavijiji za kutupilia mbali kilimo cha mazao kwa mimea isiyowafaidi. Anawaambia,

> ... Leo hii mnataka kuifuja zaidi kwa upanzi wa maua yasiyowafaidi. (uk.114)

Hali kama hii ndiyo iliyoshuhudiwa katika mataifa yanayoendelea baada ya kujinyakulia uhuru hivi kwamba mimea isiyo ya chakula ndiyo inayoenziwa kwani inasafirishwa nchi za ughaibuni na kuleta mapato mengi ikilinganishwa na mimea ya chakula ndiposa matatizo ya njaa yanaendelea kushuhudiwa. Nellemann na wenzake (2009:33) wanaeleza kuwa, mazingira asilia ni chanzo cha uzalishaji wa chakula kupitia kuwepo kwa maji,rutuba,mchanga,hali nzuri ya hewa na wadudu wanaochangia katika mchakato mzima wa ukuaji wa mimea. Wakati ardhi inapozorota, miji ikiendelea kupanuliwa na ubadilishaji wa kilimo kutoka kilimo cha mimea ya chakula hadi kilimo cha mimea isiyo ya chakula kama vile mimea ya nishati, patatokea upungufu wa chakula kutoka asilimia 8 hadi asilimia 20 kufikia mwaka wa 2050 ikiwa jambo la dharura halitafanywa.

### 4.3.2 Athari kwa wanyama na viumbe wengine

Wanyama na viumbe wengine huathirika zaidi licha ya kwamba mchango wao katika uharibifu wa mazingira ni kitu kisichodhaniwa. Mifugo huwa na taabu kupata lishe na maji kwa sababu ya kukauka kwa nyasi kutokana na ukame. Wanyama wanaotegemea majani pia wanataabika endapo miti inakatwa na hata vichaka kuondolewa kwa minajili ya makazi ya mwanadamu na maendeleo yake kiuchumi.Mwisho wa haya yote ni vifo ambavyo vinazorotesha uchumi wa wanajamii ambao tegemeo lao kubwa liko kwenye mifugo.Nakuruto anapokuwa katika kijiji cha Latimbi ukingoni mwa mto Milu anaona jinsi kima cha maji kilivyoshuka hali ambayo imeawaathiri mifugo kwa kupunguza idadi yao na kusababisha kuzoroteka kwa afya pia. Mwandishi anatuchorea picha ya masaibu ya mifugo kwa maelezo kuwa,

> Kwa mbali, aliweza kuona mifugo wachache ambao ungeweza kuhesabu mbavu zao wakifyonza maji hayo yaliyokuwa karibu kwa tope tu angalaukukata kiu... (uk.108)

Uchumi wa wavuvi umeathirika pakubwa kwani tegemeo lao kubwa ni samaki ambao sasa wamepotea. Ufuoni wanathibitisha mambo si shwari kutokana na nyuso zao zilizokosa matumaini hasa badala ya kuvua samaki wanavua vidagaa. Ba Ludao anakiri kuwa Ziwa sasa halitoi samaki pamebakia vidagaa vitupu kwani samaki wamehama anasema,

> Ah! Samaki watoke wapi dadangu. Gugumaji linatatiza uvuvi na samaki wamehama. Ukame ndio huu.Maji yamepungua mno, samaki watoke wapi? (uk.106) ...wanavijiji wamesahau madhabahu yaliyohimili asili yao. (uk.107)

Kutokuwepo kwa samaki katika Ziwa kumechangiwa na kuwepo kwa viwanda karibu na chemichemi za maji. Hata ingawa hatushuhudii umwagaji wa taka za viwanda kwenye ziwa hili, tunachofahamu ni kuwa viwanda vingi huelekeza taka zake kwenye mito na hata ziwa hali inayosababisha vifo vya viumbe wengi wa majini.

Nakuruto anawakumbusha kuwa wao ndio waliosababisha samaki kuhama kwa kukosa kutunza mazingira badala yake walijiingiza katika shughuli zilzopelekea kukauka kwa ziwa hasa Ludao aliyeanzisha uchimbaji mitaro na ufujaji wa maji ya ziwa.Anawapa suluhu la upatikanaji wa samaki ambalo ni;

> Lazima mrudishie ziwa hili uhai wake kama mnataka kuvua samaki badala ya visamaki. Ni wajibu wenu kuharibu gugumaji hili kabla halijatokomeza ziwa na nyinyi wenyewe.

### 4.2.3 Athari kwa maliasili na bioanuwai

Uchafuzi wa mazingira unaposhuhudiwa, maliasili kama vile chemichemi za maji na miti ya kiasili huanza kupotea. Jamii za kiafrika zilienzi zaidi misitu kwani ilitumika maeneo ya ibada na hata wenyeji walipata tiba za kiasili humo. Umuhimu huu wa misitu ndio uliozifanya jamii nyingi kuhifadhi misitu lakini kadri idadi ya watu inapoongezeka na uchu wa mali kuwa miongoni mwa wachache tunashuhudia uharibifu wa misitu ambayo husitiri viumbe wangi na ndicho chanzo cha chemichemi ya maji. Matatizo haya ya kupenyeza kwenye maeneo oevu kwa minajili ya kujiwekea makao na majengo mbalimbali ya shughuli za kibiashara ndiyo yanayoongeza matatizo na athari zake kuwa mbaya. Wakati misitu hii inafyekwa, kunatokea ongezeko la gesi ya makaa inayoathiri afya ya binadamu na viumbe wengine.

Katika ukurasa wa 106, Nakuruto anadai kwamba mababu wa mhusika Ludao ndio waliokuwa wa kwanza kukausha ziwa Ipe kutokana na matendo yao ya kuchimba mitaro na kuyafuja maji ya ziwa kwa kunyunyiza mashamba yao.Kwa hivyo ili kurejesha uhai wao na watoto wao waliokuwa wamehamia mijini,iliwalazimu kuponya majeraha ya ziwa hili. Katika uk. 108, tunakumbana na Nakuruto akisikitikia mto Milu katika kijiji cha Latimbi. Tunasimuliwa kwamba:

> Hapa pia simanzi ilimwingia moyoni alipoona jinsi kima cha maji kilivyoshuka. Mto ambao zama zile alizofahamu ulikuwa ukirindima kwa wingi wa maji ukanawirisha miti ya kiasili kama mvile mivule, mipingo, mikuyu na mibambakofi...

Ukataji miti kwa minajili ya kuchoma makaa katika kijiji cha Maweni unasababisha ueneaji wa maeneo tambarare huku uchimbaji mchanga ukipinguza rutuba iliyostahili kuhimili mazao

mazuri. Hali hii inasababisha Wamaweni kuhamia kwenye kijiji jirani kilicho na ardhi yenye rutuba. Ardhi iliyokuwa ikiwafaa sasa imebaki mahame kwa kukosa kuzalisha chochote. Kutokana na uchimbaji mitaro ovyoovyo na unyunyizaji maji mashamba kima cha maji kimeshuka na hata kukausha ziwa ambalo linasitiriwa na miti ambayo pia imeangamizwa na wanavijiji. Misitu imeangamizwa na kueneza tambarare nao uchimbaji wa visima umesababisha kushuka kwa maji. Rutuba iliyokuwa kwenye ardhi sasa haipo bali imesombwa na maji hali inayosababisha mmomonyoko wa udongo. Nakuruto anawaeleza wanakijiji ukatili walioyafanyia mazingira yaliyositiri uhai wao anawauliza,

> ...Je, leo hii mbona mnabeba majembe kwenda kuchimba visima ili mpate vibaba vya unga? Ni kwa sababu mmefarakana na ardhi yenu. Hamkuitunza ipasavyo na badala yake mkainyonya rutuba yake na kuiacha isombwe na maji ya mvua ovyo... (uk.114)

Uchafuzi wa hewa pia huchangia katika kupunguakwa bioanuai. Kilabuko na Madete (2010:11) wanaeleza kuwa vichafuzi vya hewa vyaweza kuangukia kwenye uoto mbalimbali ikiwemo mazao ya kilimo na kuingilia mfumo wa usaniduru na uchavushaji hivyo kupunguza mavuno yatokanayo na shughuli za kilimo.Kupungua kwa bioanuai huathiri sekta za kilimo na utalii na hivyo kupunguza pato la Taifa. Kupungua kwa mavuno ya kilimo huleta njaa, hupunguza bidhaa zinazouzwa nje ya nchi na malighafi kwa ajili ya viwanda na uchumi kwa ujumla.Inaelezwa pia kuwa uchafuzi wa hewa huathiri vitu vitengenezwavyo na binadamu kwa matumizi ya kawaida.Uchafuzi wa hewa huweza kusababisha kutu na hasara kwa vitu na mali, hivyo kuathiri uchumi wa nchi.

## 4.4 Hitimisho

Athari za uharibifu wa mazingira zinamwaathiri binadamu zaidi ya viumbe wengine wote. Katika riwaya teule athari iliyokumba wanavijiji mbalimbali imewafanya kulikumbatia wazo la Nakuruto ambaye wito wake ni kuwaunganisha wanavijiji na uhai wao. Matokeo ya ushauri ni kunawiri tena kwa mazingira. Hali hii haijitokezi tu riwayani bali ni wito wa kila mwanadamu kujali mazingira ambayo ni uhai unaomsitiri.

# SURA YA TANO

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Hitimisho

Katika kutamatisha kazi hii tutangazie kwa kifupi yale yaliyojadiliwa katika sura za kwanza nne. Tutaangazia pia kufaulu na kutofaulu kwa tasnifu hasa ikiwa nadharia tete zilizotumiwa zimejitokeza katika kazi teule. Mwisho utafiti huu umetoa mapendekezo yanayotokana na utafiti tulioufanya.

### 5.2 Muhtasari

Utafiti huu ulitambua kuwa mwandishi Clara Momanyi alikuwa na nia ya kumulika juhudi zinazofanywa na mwanamke kwa ajili ya kuokoa mazingira yake. Katika misingi ya ekolojia kifeministi, riwaya ya *Nakuruto* imetuonyesha umuhimu wa kuhusisha wanawake katika masuala ya kimazingira na hata kumulika matatizo wanayopitia wanawake endapo mazingira yatazorota. Aidha, shughuli za uzinduzi ni muhimu ili jamii ipate kuelewa utunzaji wa mazingira kwa manufaa yao wenyewe. Isitoshe, jamii hukumbana na matatizo ambayo yanachangia moja kwa moja katika uharibifu wa mazingira. Katika riwaya ya *Nakuruto* mwandishi amebainisha masuala ya kibinafsi yanayopelekea wachache kumiliki mashamba makubwa na hata sehemu zenye vyanzo vya maji huku wenyeji wakibaki taabani. Mwandishi pia ameangazia swala la ukoloni lililonyima wanavijiji nafasi ya kutumia maliasili kwa faida yao wenyewe.

Mwandishi ametusawiria matatizo wanayopata wanawake kutokana na kuzorota kwa mazingira. Matatizo ya umaskini, njaa, na vifo yanamkumba zaidi mwanamke ambaye anajitwika mzigo wa malezi. Mara nyingi mwanamke hutazamwa kama mtunzaji wa watoto ndiposa lazima ajizatiti

kuhakikisha kuwa wana wamepata chakula na makazi mema hali inayowaweka katika kufanya kazi za sulubu hasa katika mashamba ya mabwenyenye ili wakidhi mahutaji yao.

Baada ya kuchunguza matatizo anayoyapata mwanamke tumechunguza pia athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira. Hatari hizi za kimazingira hazina ubaguzi kwa njia yoyote ile kwa wanaume, wanawake na watoto. Athari tulizopata ni kama vile; magonjwa hasa yanayoathiri upumuaji,kuenea kwa maeneo tambarare kutokana na ukataji miti kiholela, vifo kutokana na hewa yenye sumu, ukosefu wa chakula unaotokana na upanzi wa mimea isiyo ya chakula kama vile pamba na hata kukauka kwa chemichemi za maji yaliyo uhai wa binadamu na viumbe wengine. Pia utafiti umegundua kuwa, wanaume wameangamia kutokana na kuangukiwa na majabali wakati wa uchimbaji madini wanaponga'ang'ania kutia chakula mezani kwa familia zao. Hata hivyo kupitia kwa juhudi za mhusika Nakuruto, jamii iliweza kujizatiti kurejesha mfumo wa ekolojia kama ulivyokuwa zamani alipokuwa mtoto.

## 5.3 Kuhusu nadharia tete

Nadharia tete yetu ya kwanza ni kuhusu mchango uliotolewa na fasihi ekolojia ya kifeministi. Uwanja huu una mchango wa kuleta mapinduzi ya kimazingira haya yamethibitika kulingana na maelezo na mifano mwafaka tuliyotoa iliyotokana na juhudi alizo nazo mhusika mkuu kuwaleta wanajamii pamoja wa kike na kiume.Mhusika Nakuruto alijitokeza kama mwanamke jasiri anayeibuka mshindi kutokana na pingamizi mbalimbali anazopitia. Kuhusu athari zinazotokana na uharibifu wa mazingira, tulidhibitisha haya kwa kuangazia matatizo ya ukame njaa vifo na hata magonjwa yaliyokuwa yakiwasumbua wanavijiji.

Nadharia tete ya mwisho ilihusu uwezo walio nao wanawake wa kuleta mabadiliko ya kimazingira licha ya pingamizi za kijamii wanazopitia. Kupitia kwa mhusika mkuu Nakuruto, tumeona mabadiliko aliyoyafanya kuokoa wanavijiji kutokana na uharibifu wa mazingira. Aidha nadharia tete hii imethibitika hasa tukizingatia ushirikiano ulioletwa na Nakuruto kuweza kuwaunganish wanavijiji kumiliki maeneo yao ili maisha yao yabadilike.Nakuruto kama mwanamke aliyekuwa mstari wa mbele kuhifadhi mazingira na hata kuitwa afisa wa mazingira. Juhudi alizofanya Nakuruto zimemfanya kuwa katika nafasi nzuri ya kuleta mabadiliko hasa kupitia uzinduzi na ukombozi wa kimazingira hivyo basi kusawiri wanawake kama wenye uwezo mkubwa wa kubadilisha mazingira almuradi wanaungwa mkono.

## 5.4 Mapendekezo kuhusu utafiti zaidi

Uharibifu wa mazingira ni suala linalozungumziwa kila wakati kutokana na athari tunazozidi kuhisi kote duniani. Masuala haya tayari yamepata nafasi katika fasihi ya Kiswahili jinsi utafiti huu ulivyobainisha. Mwandishi Clara Momanyi ameonyesha ukakamavu wa kumsawiri mwanamke kama chombo cha mabadiliko ya kimazingira. Utafiti wa kimazingira ni mpana zaidi kadiri diskosi mbalimbali katika nyanja mbalimbali zinavyopenyeza katika usomaji wetu. Ni vigumu kuweza kutafitia masuala yote ya kimazingira ndiposa utafiti huu kwanza unapendekeza kuwa, lazima pawepo na utafiti wa baadaye wa kina ambao kwanza utaoanisha nadharia ya kimazingira na nadharia ya baada-ukoloni kwani ukoloni umechangia katika uharibifu wa mazingira jinsi ambavyo wakoloni katika utawala wao, walivyovuruga shughuli za Waafrika za kuyatunza mazingira.

Pili, nadharia ya fasihi ekolojia kifeministi ni ngeni na pana katika fasihi na inashughulikia maswala mengi. Utafiti huu unapendekeza kuwa utafiti wa baadaye umulike zaidi mihimili mingine ya nadharia hii ambayo haikupata kujadiliwa na hata kujitokeza katika riwaya ya *Nakuruto* ili nadharia hii ipate kupanuka na kueleweka vizuri zaidi na wasomo wa fasihi ya Kiswahili. Baadhi ya mikabala ya kifasihi kiekolojia ambayo inaweza kutafitiwa ni fasihi mazingira ya kieneo, Kiafrika na Kimagharibi. Pia utafiti wa baadaye unaweza ukachukua mwelekeo wa kilinganishi kwa baadhi ya mikabala hii.

Tatu, swala la wanawake kujihusisha katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira sio jambo geni kwani wanawake wengi wa kiafrika wamejihusisha katika shughuli za upanzi wa miti ingawa hawajaangaziwa na jamii zao hivyo basi utafiti huu unapendekeza kuwa wasanii wengi wajitose katika nyanja za uandishi wa fasihi za kimazingira na kulimulikia zaidi swala la wanawake kupigania mazingira mema ya jamii zao. Pia, wasanii wa fasihi washughulikie zaidi hali ya kudorora kwa mazingira na suluhu katika ili ujumbe ufikie jamii nzima.

## Marejeleo


Ameir, S. (2010) 'Shein aieleza Afrika: Msidharau maarifa ya asilia katika kukabiliana Na changamoto za mazingira zinazolikabili Bara la Afrika' katika *Jarida la Umaskini na Mazingira.*Toleo la 8:3-4 Penplus Ltd: Tanzania.

Buckingham, S. (2003) Ecofeminism in the 21st Century. *The geographical Journal 170, 2:146-154*

Cheche, B. (2009) 'Utu wa Mtu Unadhihirika Katika Utunzaji wa Mazingira' katika *Jarida la Umaskini na Mazingira.* Toleo la 7:6-10 Penplus Ltd: Tanzania

Dagny, k. (1997) 'Eco -News from Across the World Ecofeminism in the Nordic Countries' in *Ecotheology* 2:100-108

FAO (2011) *State of the World's Forests.*Food and Agriculture Organization of the United Nations, Rome.

Gaard, G. (Ed) (1993) *Ecofeminism: Women, Animals, Nature.*Temple University Press: Philadelphia.

Garrard, G. (2007) 'Ecocriticism and Education for Sustainability' in *Pedagogy: Critical Approaches to Teaching Literature, Language, Composition, and Culture.* Volume 7(3):359-386. Duke University Press

Glotfelty na Fromm (1996) *The ecocritical reader.* New York: Routledge

Grazebrook, T. (2002) 'Karen Warren's Ecofeminism' in *Ethics & the Environment* 7(2 ). Indiana University Press: Bloomington.

Hitt, C. (2004) Ecociticism ana the Long Eighteenth Century in *College Literature* 31(3):123-146

Joekes, et.al (1994) 'Gender, Environment and Population', in Dharam Ghai (ed.), *Development and Environment: Sustaining People and Nature*, Blackwell Publishers Oxford.

Kilabuko, na Madete, (2010 :) 'Uchafuzi wa Hewa Unavyoathiri maendeleo ya Jamii' katika *Jarida la Umaskini na Mazingira* Toleo la 7:10-12 Penplus Ltd: Tanzania

Kokahvah, Z. D. (2007) 'Women Who Know Things: African Epistemologies, Ecocriticism, and Female Spiritual Authority in the Novels of Toni Morrison' in the *Journal of Pan African Studies*, vol. 1, no. 7, March 2007

Lahar, S. (1991) 'Ecofeminist Theory and Grassroots Politics' in *Hypatia* 6(1), 28

Maarugu, K. E. (1992) *Adui wa Umma*. EK International Publishers: Tanzania

Maembe, na Mudiguza, (2010) 'Majanga yanavyochangia kuongeza umaskini: Maporomoko ya ardhi pamoja na mafuriko ya Same na Kilosa na madhara yake katika mazingira, kijamii na kiuchumi' katika *Jarida la Umaskini na Mazingira.* Toleo la 8:5-6. Penplus Ltd: Tanzania

Merchant, C. (1980) *The Death of Nature: Women Ecology and Scientific Revolution.* Harp SanFransisco: San Fransisco.

Merchant, C. (1989) Ecological Revolutions: Nature, Gender and Science in New England, University of North Carolina Press.

Mies, M and Shiva, V. (1993) *Ecofeminism*, Zed Books: London.

McFague, S. (1993) *The Body of God: An Ecological Theology*. Minneapolis: Fortress.

Mohamed, A. S. (2001). *Jicho la ndani.*Nairobi : Longhorn Publishers.

Momanyi, C. (2009) *Nakuruto*. Nairobi : Longhorn Publishers.

Moore, N. (2008) 'Eco/Feminism, Non-Violence and the Future of Feminism' in *International Feminist Journal of Politics*, 10(3), 282–298 Taylor and Francis Group: Routledge

Muthuki, J. M. (2006) Rethinking Ecofeminism: Wangari Maathai and the Green Belt Movement in Kenya. Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kwazulu- Natal (Howard College Campus) katika www,academia.edu/6253747/The-Green_Belt_Movement_Ecofeminist of_Wangari_Maathai

Nalunnakkal, G. (2004). 'Towards an Organic Womanism: New Contours of Ecofeminism in India' *Asia Journal of Theology*18 (1), 51-68

Nellemann, et.al (Eds) (2009).*The environmental food crisis – The environment's role in Adverting future food crises.*A UNEP rapid response assessment. Birkeland Trykkeri AS: Norway.

Nwagbara, U. (2010) Poetics of Resistance: Ecocritical Reading of Ojaide's Delta *blues & Home Songs* and *Daydream of ants and other poems. African Study Monographs*, 31(1), 17-30

Ojomo, P. A. (2011) 'Environmental Ethics: An African Understanding' in *the Journal of Pan African Studies*, vol.4 (3), March 2011

Osoro, M. (2003) Uhakiki wa Riwaya Za Ahmed Mohamed Katika Misingi ya Kifemini Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Rigby (2007) 'Ecocriticism' in Julian Wolfreys (ed.) *Introducing Criticism in the Twenty-First Century*. Edinburgh University Press: Edinburgh.

Reuther. R. (1997) 'Ecofeminism: First and Third World Women' in *Journal of Religion, Nature &The Environment 5(2*), 72 -83

Schulz, B. U. (2001:201-203) 'Habari za Miti na Mitishamba Miongoni mwa Wamijikenda na Waswahili' in *Swahili Forum* viii 201-203

Shiva, V. (1988) *Stayingalive: Women, ecologyand development*. ZedBooks: London.

Slovic, S. (2009). 'A booklist of international environmental literature' in *World Literature today online*.Oklahoma: Oklahoma State University

Sturgeon, N. 1997) *Ecofeminist Natures: Race, Gender, Feminist Theory, and Political Action*. New York: Routledge.

Taylor, B. (2005) *Encyclopedia of Religion and Nature*. New York: Continuum

Wa Mberia, K. (2001) Bara *Jingine*. Marimba Publications : Nairobi.

____________ (2001) Kifo *Kisimani*. Marimba Publications : Nairobi.

Wamitila, K. W. (2003) *kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Focus Publishers: Nairobi.

Warren, K. (2000) *Ecofeminist Philosophy: A Western Perspective on What It Is and Why It Matters*. Rowman & Littlefield Publishers, Inc: New York.

Warren, K. (1997) *Ecofeminism: Women, Culture, Nature*. Indiana University Press: Bloomington.

Warren, K. and Cheney, J. (1991) 'Ecological Feminism and Ecosystem Ecology' in HypatiaVol. 6 (1) 179-196

Vierke, C. (2007). 'Of plants and women.A working edition of two Swahili plant poems.'*Swahili forum 14,* 27-80.

UNCED(1992)Agenda21http://sustainabledevelopment.un.org/content/documents/Agenda21.pdf

UNDP (2004).*Human Development Report 2001: Making New Technologies Work for Human Development.* United Nations Development Programme, New York, NY

UNDP (2005) *Human Development Report 2005: International Cooperation at a Crossroads.* United Nations Development Programme, New York, NY

World Bank (1992).World Development Report: Development and the Environment, Oxford University Press, New York,

Viambatisho

Kiambatisho a: Delta Blues

This share of paradise, the delta of my birth,
Reels from an immeasurable wound.
Barrels of alchemical draughts flow
From this hurt to the unquestioning world
That lights up its life in a blind trust.
The inheritance I sat on for centuries
Now crushes my body and soul…

My nativity gives immortal pain
Masked in barrels of oil—
I stew in the womb of fortune.
I live in the deathbed
Prepared by a cabal of brokers
Breaking the peace of centuries
& tainting not only a thousand rivers,
My lifeblood from the beginning,
But scorching their sacred soil was debauched
By prospectors, money-mongers?

My birds take flight to the sea,

The animals grope in the burning bush... Nwagbara (2010:24)

Kiambatisho b: The AT & P, Sapele

When I first entered the AT & P

on excursion from St. George's,

it was next to the largest sawmill

on earth...

The planks smelt fresh,

Sardine-packed for export;

they came in raft by water...

When decades later I went home

to the delta of hardwood,

a big clearing welcomed me... Nwagbara (2010:25)

Kiambatisho c: Song of Ocol

Woman of Africa

Sweeper

Smearing floors and walls

With cowdung and black soil

Cook, ayah, the baby on your back

Washer of dishes,

Planting, weeding, harvesting

Storekeeper, builder

Runner of errands,

Cart, lorry, donkey…

Woman of Africa

What are you not? Warren (2000:9)